Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

لا إله إلا الله محمد رسول الله

# Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

**Nukuu ya Qur'an Tukufu**

Allah Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya Makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya Makhalifa wale wa kabla yao... (24:56)

JUZU 78 No. 194 | SHAB - RAMADH 1439 AH | JUNI 2018 | IHSAN 1397 HS | BEI TSH. 500/=

# Khalifa Mtukufu Awakumbusha Waaminio Ramadhan Mwezi wa Kuchuma Taqwa

Baada ya *Tashahhud, Taawwudh* na *Surat Faatihah*, Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisoma aya 184 ya sura Al Baqarah:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُتِبَ عَلَيۡكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ

"Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga saumu kama walivyolazimishwa wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu." (2:184)

Hudhur (a.t.b.a) alisema: Kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu na baraka Zake, mwaka huu pia sisi tumebahatika kushuhudia mwezi mtukufu wa Ramadhan. Katika mwezi huu Waislamu wengi duniani kote wanahudhuria misikitini kusali na kumwabudu Mwenyezi Mungu. Aya hii niliyoisoma mbele yenu inatukumbusha ya kwamba kusudio kuu la kufunga saumu ni kupata kumcha Mungu. Nalo lilikuwa kusudio la kuwalazimisha watu wa kabla ya Uislamu.Sisi Waahmadiya tuna jukumu kubwa la kufahamu na kuelewa falsafa ya saumu na inabidi tujitahidi kuyapata yale unayolenga mwezi huu mtukufu, yaani kupata Taqwa na kuzidi pia. Kuna aya zingine zinatuonesha umuhimu wa mwezi wa Ramadhan na kiini cha Aya zote hizi ni kufanya bidii ili tupate kumcha Mungu. Mwezi huu haswa tunatakiwa kujitahidi katika kufuata mafundisho ya Mwenyezi Mungu na kumuabudu ipasavyo ili mambo haya yawe sehemu ya maisha yetu mazima.

Katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhan tutakapofanya jitihada ya kuupata ucha Mungu, tutakuwa tumepata jazba ya kufanya ibada zaidi na kujiepusha na mambo mabaya. Na tunapokuwa sisi hatujiepushi na mambo hayo mabaya basi tutakuwa hatutimizi kusudio la ibada ya saumu. Ikiwa katika saumu mtu atakuwa na tabia ya kiburi, ubinafsi na kujipendelea basi tabia hii haitakuwa ya kiucha Mungu. Na vile vile mtu baado kama atakuwa na tabia ya kugombana na kutukana basi hii

*Endelea uk 2*



*Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akitoa hotuba ya Ijumaa ndani ya Baitul Futuh, msikiti uliopo jijini London na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.*

# Tende Na Faida Zake

Na **Dkt. Pazi Kitabu**

Tende ni tunda lenye historia kubwa na pana katika maisha ya binadamu. Wakati vitabu vya kale vinaandika Nabii Issa (A.S) kuzaliwa kwenye mitende, Mtume Muhammad (S.A.W) alitumia tende kuwa chakula kikubwa si katika mwezi wa Ramadhani tu bali katika maisha ya kila siku alipendelea kula tende mara nyingi.



Pamoja na kuwa tende kama tunda kwa udogo wake inaweza kutosheleza mahitaji makubwa ya chakula muhimu kwa binadamu, hivyo kupunguza kubeba au kutumia chakula kingi kama ugali, ubwabwa, magimbi na mihogo hususan katika mwezi huu wa Ramadhan. Tende ina manufaa makubwa ya kiafya kulinganisha vyakula vingine na hapa nitaeleza machache.

***1. Kupunguza shinikizo la damu***

Tende ina madini ya Magnesi (Magnesium) kwa wingi ambayo yanapunguza shinikizo la juu la damu. Utafiti wa kisayansi juu ya madini haya umeonyesha kuwa yana uwezo mkubwa wa kupunguza tatizo la shinikizo la damu kwa kiwango kikubwa na hii inathibitishwa na ukweli kuwa dawa ya Magnesi Salfeti (Magnesium Sulphate) ndiyo inayotumika kutibu maradhi mengi hususan kina mama wanaopata

*Endelea uk 3*

# Ziara Ya Kufana Ya Amir Sahib Tabora Na Kigoma

Na **Mahmood K. Mubiru**

Kiongozi wa Jumuiya ya Ahmadiyya nchini Tanzania, Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry ameleta msisimko wa aina yake katika Jamaati za Tabora na Kigoma alizozitembelea 22-03-2018 hadi 04-2018.




*Amir na Mbashiri Mkuu akihutubia Jalsa Salana ya mkoa wa Tabora*

Ilikuwa ni ziara iliyojaa baraka tele na mafanikio sahib aliwahimiza makubwa. Akiwa Tabora yenye sifa ya kuwa kituo cha kwanza alipoanza kazi ya Ubashiri Sheikh Mubarak Ahmad 1934, Amir sahib aliweza kuhudhuria Jalsa ya mkoa huo. Akizungumza na wanajamaat Amir

*Endelea uk 4*

**Jibu Kwa Sheikh Sawafi Muibadhi Wa Nchini Oman - Uk. 5**

# Mapenzi ya Mungu

## Maoni ya Mhariri

### Miaka 15 Ya Baraka Zisizohesabika Na Zinazoendelea – Inshaallah

Tarehe 22 Aprili 2003 ni siku muhimu na ya kihistoria kwani ndio siku alipochaguliwa na Allah kwa kupitia mikono ya waaminio Hadhrat Mirza Masroor Ahmad – Allah Aimarishe mkono wake, kuwa Khalifatul Masih V. Toka achaguliwe dunia imeshuhudia maana ya kuwa Khalifa wa Allah huku falsafa ya Kitabu cha Allah na kututakasa kukiendelea. Tunatoa shukurani kubwa kwa Allah Kutuwezesha kuona kwa macho yetu dhihirisho la pili kama alivyoahidiwa Masihi Aliyeahidiwa - Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.

Baraka na neema zilizopatikana katika miaka hii kumi na tano ni nyingi na ni muhali kuzihesabu. Tunajitupa kwa Kizingiti cha Allah tukishukuru neema kubwa tuliyoipata sisi tuliokubali kuingia katika Safina hii iliyoundwa na Mwana wa Kiroho wa mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. Katika miaka hii tumeshuhudia baraka na mafanikio makubwa. Kuyataja yote sio tu kwamba ni vigumu lakini haiwezekani. Tutajitahidi baraka hizo ikiwa ni alama ya kutoa shukurani kwa Allah na ni mafundisho ya Allah kwamba Neema za Allah tuzidhihirishe.

- Uanzishaji wa taasisi ya kukusanya kazi za Khalifatul Masih wa IV Hadhrat Mirza Tahir Ahmad r.h.
- Ujenzi wa msikitimkubwa kuliko yote barani Ulaya – Baitul Futuh.
- Uendelezaji wa Taasisi ya Moyo ya Tahir.
- Kupatikana Wanajamaat 15,000 kujiunga na nidhamu ya Wasiyyat kabla ya mwisho wa karne ya kwanza ya mpango huo.
- Uanzishaji wa Taasisi ya kushughulika na masuala ya ndoa – Nazarat-e-Rishta Nata
- Tuzo ya Amani – 'Ahmadiyya Peace Prize'
- Uanzishaji MTA3 kwa wasemaji wa Kiarabu, MTA Afrika, MTA kwa lugha za Ulaya, MTA kwa ajili ya Marekani.
- Taasisi ya Noor kuchapisha vitabu vya Hadith.
- Ongezeko la mitambo ya uchapishaji magazeti na vitabu.
- Uanzishaji wa vijiji vya mfano.
- Ujenzi wa misikiti katika miji mikubwa ya Uingereza.
- Ardhi kwa ajili ya Jalsa Salana – Hadeeqatul Mahdi.
- Uanzishaji wa Jamia za kimataifa Kanada, Ujerumani, Uingereza na Ghana.

Kama tulivyosema mwanzoni, ni vigumu kuzitaja baraka zote. Tunashukuru Allah kwa neema hizi na tunamuomba tuendelee kuishika kwa nguvu zetu zote kamba ya Ukhalifa kwani uhai wetu umo katika msimamo huo.

# Ramadhani na Taqwa

*Kutoka uk. 1*

pia haitakuwa tabia ya kiucha Mungu.

Hudhur (atba) alieleza: Baadhi ya watu hufunga saumu kwa ajili ya kujionesha tu. Kijana mmoja alikuwa anaeleza katika kipindi kimoja cha 'TV' ya kwamba yeye alikuwa anakula daku na jioni alikuwa anafuturu kwa futari za aina mbalimbali lakini haya yote aliyafanya kwa sababu ya msukumo wa jamii yake iliyokuwa na kawaida ya kufunga saumu lakini wakati wa mchana alikula kama kawaida. Kijana huyu akaongeza ya kwamba hivi hivi ndivyo wanavyofanya vijana wengi wengine.

Hudhur (atba) akakazia ya kwamba hii ndiyo hali halisi ya saumu ya baadhi ya watu yaani mtu kama ameacha kula na kunywa kutwa nzima bila ya kujali sala wala kufuata yale yaliyoamrishwa, na yale yaliyokatazwa, basi lile kusudio la saumu halitafikiwa.

Sisi Waahmadiya tuna jukumu kubwa mabegani mwetu la kutekeleza ibada hii ya saumu sawasawa kwa kuzingatia ucha Mungu ni nini na kuna njia gani ya kuupata.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) katika sehemu mbalimbali ameeleza kuhusiana na ibada ya saumu na jinsi ya kupata ucha Mungu.

Mwaminio wa kweli anatakiwa kulifanya kila jambo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu na hii ndiyo tofauti pekee kati ya mwaminio na kafiri.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alisema: Kama Kuna Jumuiya yoyote isiyokuwa na Taqwa mbele ya Mwenyezi Mungu, msaada Wake hautakuwa pamoja nayo. Taqwa ndiyo msingi wa mafundisho ya vitabu vyote vitakatifu vikiwemo Torati na Injili. Mwenyezji Mungu katika neno hili moja tu la Taqwa Amejumuisha matakwa yake na radhi yake yote.

Kisha akasema: "Kama mnataka maombi yenu yapokelewe basi tembeeni katika msingi wa Taqwa, kwa sababu ndiyo msingi wa sheria zote za Quran. Madaraja ya kupata ucha Mungu ni mengi lakini kama mtu akijitahidi, huweza kupata madaraja ya mwanzo na anapoendelea kupita katika madaraja hayo kwa nia safi basi hufikia madaraja ya juu zaidi.

Mwenyezi Mungu Anasema:

Kwa yakini, Mwenyezi Mungu Huwakubalia wale walio wacha Mungu tu (5:28). Yaani hii ni ahadi yake, naye hafanyi kinyume na ahadi zake. Basi hili ni sharti la kukubaliwa maombi. Yule anayeghafilika na tena anataka maombi yake yapokelewe, basi ni mtu mjinga.

Kwa hiyo kila mmoja katika Jumuiya yetu anatakiwa atembee katika njia halisi ya ucha Mungu ili tuweze kupata ladha ya kupokelewa kwa maombi yetu na imani iongezeke.

Kisha akasema tena: Kwa ajili ya wacha Mungu na watawa kuna ahadi nyingi. Je Kuna ahadi iliyo nzuri zaidi kuliko hii ya kwamba Mwenyezi Mungu Mwenyewe Ndiye Atakuwa Mlinzi na Msaidizi wake? Watu wale wanaodai kuwa karibu na Mungu wakati hawana Taqwa na badala yake wanaishi katika maisha ya ufisadi na ufasiki, wao ni waongo.

Mwenyezi Mungu Anasema:

Kwa yakini Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wale wamchao na wale wafanyao wema (16:129), yaani Anawasaidia. Kumbukeni msaada wake hawaupati walio wachafu na mafasiki.

Hadhrat Khalifa mtukufu (atba) alisema: Sisi tunatakiwa kusoma sana aya hii na kuizingatia:

Yule amchaye Mungu, Humjaalia njia ya kuokoka na Humpa riziki kutoka mahali asipopategemea. (At-Talaaq 65:3-4)

Kisha Masihi Aliyeahidiwa akaendelea kusema: Mcha Mungu katika nyumba yake ndogo hupata furaha ya kweli ambayo mtu wa dunia mwenye tamaa hawezi kuipata hata katika kasri la kifahari. Kadri mtu anavyozidi kuipata dunia ndivyo anavyozidi kupata mitihani. Basi kumbukeni furaha haswa haipati anayetafuta dunia. Msifikiri kuwa wingi wa mali, nguo za fahari na vyakula vizuri vinaweza kuwa sababu ya furaha ya kweli. Haiwezekani. Bali msingi wa furaha ya kweli haswa ni ucha Mungu.

Taqwa ina matawi mengi yaliyoenea kama nyuzi za wavu wa buibui. Na sehemu iliyo dhaifu zaidi inahusiana na ulimi. Wakati mwingine mtu husema jambo akiwa amesahau Taqwa. Bwana mmoja mcha Mungu alikaribishwa nyumbani kwa mtu wa dunia. Ulipofika muda wa chakula, mwenyeji akamwagiza mtumishi wake alete sahani aliyoinunua wakati wa hija ya kwanza. Alipoileta akamwagiza kuleta sahani nyingine aliyoinunua wakati wa hija ya pili. Nayo alipoileta akamtuma tena kuleta sahani nyingine ya tatu aliyoinunua wakati wa hija ya tatu. Yule bwana mgeni akasena: Wewe ni mtu wa kuhurumiwa sana. Kwa usemi wako huu umeharibu hija zako zote tatu. Kusudio lako la hayo yote ni kutangaza kuwa wewe umewahi kuhiji mara tatu. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu Amefundisha ulimi unatakiwa utumike kwa uangalifu mkubwa.

Hudhur (atba) akasema: Katika kufunga saumu mtu anatakiwa azidi katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu na apunguze kuzungumza mambo yasiyofaa ili kupata kusudio la saumu na kuufikia ucha Mungu.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema: Wema una sehemu mbili, moja ni faradhi na nyingine ni ya nafal. Faradhi ni ile ambayo ni ya lazima kama vile mtu anavyolipa deni au malipo ya wema ni kufanya wema. Pamoja na faradhi hizi, kila wema una nafali zake. Yaani kufanya wema zaidi ya ule anaostahiki mtu. Yaani malipo ya hisani ni kutenda hisani zaidi ya ile iliyofanywa. Mambo haya ni baadhi ya yale yanayozikamilisha faradhi. Imesimuliwa katika hadithi ya kwamba vitendo vya faradhi vya Mawalii wa Mwenyezi Mungu hukamilishwa na nafali zao. Yaani zaidi ya kutoa zaka hutoa sadaka na michango mingine pia.

Mwenyezji Mungu Mwenyewe Anakuwa rafiki wa watu kama hawa. Mwenyezji Mungu Anasema, urafiki Wake na mtu unafikia hatua ya kwamba Yeye mwenyewe Anakuwa mkono, mguu na hata ulimi wake anaozungumizia.

Kisha Hadharat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alisema: Tabia ya mwaminio wa kweli ni hii ya kwamba, kila anapopata mafanikio anahisi haya na humtukuza Mwenyezi Mungu kwa sababu Yeye ndiye Aliyetoa fadhili zake na ndivyo anavyoendelea kusonga mbele. Naye husimama imara katika kila mtihani anaopata. Kwa dhahiri mafanikio ya mwaminio na kafiri yanashabihiana lakini mafanikio ya kafiri yanampeleka kwenye kiza kwa sababu yeye haelekei kwa Mwenyezi Mungu bali anazifanya juhudi, akili na uwezo wake kuwa Mungu. Upande mwingine mwaminio huelekeza haya yote kwa Mwenyezi Mungu na kujenga naye uhusiano mpya. Hivyo kila anapopata mafanikio anazidi katika ukaribu Naye na kupata mabadiliko mema mapya.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alisema: Mwenyezi Mungu Hutengeneza orodha ya vitendo vya mwanadamu basi mtu anatakiwa aweke orodha ya vitendo vyake vya kila siku na atafakari kwa kiasi gani amezidi katika kutenda vitendo vizuri. Hali yake ya leo haitakiwi ilingane na ile ya jana. Yule ambaye hesabu ya vitendo vyake vya leo inalingana na ile ya jana bila shaka amepata hasara. Lazima kila siku vitendo vyake vyema viongezeke. Kama mtu ni mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na kuwa na yakini naye, basi yeye hataangamia bali maelfu ya watu wanaokoka na mabalaa mengi kwa sababu yake.

Mwenyezi Mungu Atujaalie katika mwezi huu wa Ramadhani tufunge saumu kwa kuzingatia Taqwa nao uwe wenye baraka tele. Hususan maombi makhsus yanatakiwa kwa ajili ya nchi ya Pakistan kwa sababu hali inazidi kuwa mbaya. Mwenyezi Mungu Awahurumie Waislamu wote na Awajaalie akili ya kumtambua Imamu wa zama. Kila siku duniani kuna habari ya kutokea kwa Vita Kuu. Mataifa makubwa yanaelekea kwenye vita hivyo. Mwenyezi Mungu Awanusuru Waislamu wote na hususan Waahmadiya kutokana na athari zake mbaya na pia Awaokoe wanadamu wengine.

Mwenyezi Mungu Ajaalie hali ya watu wamtambue Yeye ili wanusurike na maangamio ya Vita hivyo. Aamin.

BODI YA UHARIRI

**Msimamizi:** Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
**Mhariri:** Mahmood Hamsin Mubiru.
**Kompyuta:** Sheikh Abdulrahman M. Ame.
**Mchapishaji:** Sheikh Bashart Ur Rehman
**Msambazaji:** Mwl. Omar Ali Mnungu
**Wajumbe:**
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
**Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.**
**Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Email: mapenziyamungu36@gmail.com**

# Subhana'llah!! 'Waislamu' Wavunja Msikiti Pakistani

Usiku wa tarehe 24 Mei ya mwaka 2018, kwa mara nyingine tena Taifa la Pakistani limeandika historia mbaya ya Nchi hiyo yenye wakazi wengi Waislam ambao wana msimamo mkali dhidi Waislam wafuasi wa Jumuiya ya Ahmadiyya.

'Waislam' hao wakipewa ulinzi wa askari wa Serikali walivamia msikiti huo na kuuvunja pamoja na nyumba iliyo karibu na msikiti ambayo pia ni mali ya Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya katika mji wa Sialkot nchini Pakistani. Hakuna mtu aliyekuwepo wakati wa uvamizi huo haramu na hivyo hakuna majeruhi yaliyopatikana. Tukio hilo ambalo limeelezwa ni la kushangaza haswa kufanywa na 'Waislam' limeleta wasiwasi mkubwa juu ya nini kitafuata baada ya tukio hilo ambalo linaweza shusha ghadhabu ya Allah kwa nchi hiyo.

Msikiti huo wa kihistoria ambao una umri zaidi ya miaka mia moja, pia uliwahi kutumiwa na mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya ambaye pia ni Masihi wa zama za mwisho Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (AS) kufanya ibada zake za sala na Itqaf.



*Masjid Mubarak uliopo mjini Sialkot nchini Pakistani, pichani kabla na baada ya kuvunjwa.*

Picha mbali mbali za video toka mitandao ya kijamii na vyombo mbalimbali vya habari duniani zimeonyesha askari wa Taifa hilo wakisimamia zoezi hilo na kutoa msaada wa uharibifu huo wa msikiti kitu kinachoonyesha kuwa uvunjwaji huo wa msikiti una baraka zote za Serikali ya Pakistani.

Katika taarifa iliyotolewa na Amir Jamaat Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaundry, alisema kuwa msikiti huo unaoitwa Masjid Mubarak una historia kubwa kwa Jumuiya ya Ahmadiyya duniani, Seydna Ahmad (AS) alikuwa akisali sala zake humo alipokuwa anaishi mjini Sialkot. Pamoja na kuibomoa minara yake na mimbari pia wamebomoa ile nyumba ambayo Hadhrat Masih Mau'ud (AS) alikuwa anaishi wakati ule, ilieleza taarifa ya Amir Jamaat Tanzania.

Wapinzani wanaokadiriwa kuwa zaidi ya elfu moja walianza kubomoa msikiti na nyumba na waliendelea na kazi hiyo hadi asubuhi, kwa kweli hali ni ngumu kwa wanajumuiya wenzetu wanaoishi Pakistani na yatupasa tuwakumbuke katika maombi yetu katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani ili Mwenyezi Mungu awalinde katika shari zote, ilimalizia taarifa ya Amir Jamaat Tanzania.

Hayo na mengine mengi ni muendelezo wa mlolongo wa mateso na usumbufu mkubwa wanaopata wafuasi wa Jumuiya hii duniani hususan nchini Pakistani.

Sheria kandamizi na kizandiki zilizowekwa dhidi Waislam wa Jumuiya ya Ahmadiyya na Serikali na zinachochewa na husuda, chuki na kila aina uonevu zimekuwa zikiendelea nchini Pakistani kila kukicha. Tunamuomba Allah awaongoze viongozi wa Pakistani ili waache dhuluma dhidi ya Waislam Ahmadiyya na watu wa dini zingine pia. Amin.

# Tende na Faida Zake

*Kutoka uk. 1*

kifafa cha mimba ambacho kinaambatana na shinikizo kubwa la damu.

Pamoja na kufanya kazi ya kuzuia kifafa cha mimba, Magnesi Salfeti (Magnesium Sulphate) inashusha shinikizo la damu kwa ufanisi mzuri zaidi. Madini ya Magnesium yapo kwa wingi kwenye tende. Tahadhari kwa wapenzi wasomaji ni kwamba, usitumie tende kutibu kifafa cha mimba mpeleke hospital akapate Magnesi Salfeti (Magnesium Sulphate) kwa njia ya sindano itayofanya kazi kwa haraka zaidi.

***2. Kupunguza hatari ya kiharusi***

Utafiti uliofanywa na kutolewa katika machapisho saba kwa muda wa miaka 14 umeonyesha kuwa hatari ya kiharusi hupungua kwa asilimia 9, ikiwa mtu atatumia milligram mia moja za Magnesi (Magnesium) kwa siku, ambazo hupatikana kwa wingi na urahisi kwenye tende. Utafiti na machapisho haya unaweza kuvipata kwenye "American Journal of Nutrition".

Tufahamu kuwa shinikizo la damu lisipotibiwa kwa muda mrefu au hata mfupi linaweza kusababisha mtu kupata kiharusi (Kupooza viungo vya mwili) na hivyo kuwa mlemavu na utegemezi. Hali hii inatokana na ubongo kuathiriwa kutokana na kiharusi hicho. Aidha tuelewe kuwa ubongo ndiyo kiungo muhimu kinachosimamia ufanyaji kazi wa viungo vingine vya mwili. Ukitumia tende unaweza kujikinga na kiharusi na tukumbuke kuwa mtu akipata kiharusi aende hospital kwa msaada mwingine wa kimatibabu. Kwa hiyo kinga ya kiharusi ndiyo njia bora zaidi kwa afya ya binadamu.

***3. Afya ya mimba na uzazi***

Tende imeonyesha kuleta matokeo mazuri ya ujazito na uzazi. Utafiti wa kisayansi kwa wanawake wajawazito 69 waliofuatiliwa kwa miezi 13 umeonyesha kuwa matumizi ya tende kwa wiki 4 za mwisho kabla ya uchungu kuanza hupunguza haja ya kuanzishiwa uchungu au kuupa nguvu uchungu na pia kuleta matokea mazuri kwa wazazi baada ya kujifungua.

Utafiti huo uliofanywa na Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia nchini Marekani unatoa fursa kwa tafiti zaidi katika hili kujua kama virutubisho vya tende vina athari ya moja kwa moja kwa matokeo ya akina mama hao. Aidha inashauriwa kwa mama mjamzito si vibaya kutumia tende kama sehemu ya chakula chake kama ikiwa hana shida nyingine kama kisukari n.k.

***4. Kupunguza hatari ya saratani kwa njia ya chakula***

Tende ina nyuzi nyuzi nyingi ambazo husaidia kwa kiwango kikubwa kufanya mmeng'enyo wa chakula kwa haraka zaidi



*Mwalimu Nyerere akipata futari na Wazee*

na kusaidia upatikanaji wa choo kilicho laini. Tufahamu kuwa pamoja na sababu zingine, saratani ya njia ya chakula husababishwa na kukosa choo kwa muda mrefu na huu hupekelekea kutuwama kwa sumu mbali mbali zilizopaswa kutolewa kwa njia ya haja kubwa. Kwa kupata choo kunakosababishwa na ulaji wa tende kunapunguaza hatari ya mtu kupata saratani za utumbo.

Aidha mtu anapokosa haja kubwa au kupata choo kigumu, kunapelekea kutumia nguvu nyingi kujikamua chooni na hali hii inaweza sababisha kupasua mishipa midogo ya damu na kupata tatizo la usubi (haemerroids). Mtu anapata choo chenye damu nyepesi au choo chenye kuchanyika na damu, na kupungikiwa damu. Vile vile kuna hatari ya mtu kupata maradhi ya ngiri pia ikiwa mtu ana shida nyingine ya kimaumbile ya mishipa damu kama ya kichwani au ya shingoni, inaweza kupasuka na kuhatarisha maisha kwa haraka sana kama atakosa msaada. Kwa ujumla suala la kupata choo kigumu au kukosa choo linaweza kuzuiwa na vyakula vya nyuzi nyuzi hususan tende kukinga maradhi yaliyoelezwa hapo juu.

***5. Huimarisha kinga ya mwili***

Kama tulivyoona hapo juu kuwa, tende ina madini mengi ya Magnesi (Magnesium). Madini yanasaidia mwili kupambana na magonjwa. Viashiria vya mwili kuwepo kwa ugonjwa kama C-reactive protein, TNF alpha na IL6 huwa vinapungua kama si kumalizika kabisa iwapo Magnesi (Magnesium) itaongezeka mwilini. Utafiti pia umeonyesha kuwepo kwa magnesium husaidia kuponya maumivu ya viungo (arthritis) na kusahau (alzhemiers).

***6. Kuongeza afya ya ubongo***

Tende pia ina kirutubisho cha Vit B6 ambacho kinasaidia kuongeza ufanisi wa ubongo na kuimarisha afya ya akili ya mtu. Utafiti uliochapishwa kwenye jarida la madaktari wa magonjwa wa ndani nchini Marekani umeonyesha kuwa Vit B6 inasukuma uwezo wa ubongo kufanya kazi na kutoa matokea mazuri ya kitendaji.

Faida za tende zipo nyingi hasa ukizingatia kuwa tunda hili lina virutubisho vingi sana ambavyo ni mara chache kuvipata kwa matunda mengine. Madini kama ya Potasiamu (Potasium), Shaba (copper), Manganizi (Manganese) n.k. yana faida nyingi kwa binadamu ikiwa ni pamoja na kuimarisha mapigo ya moyo

Aidha tende ina sukari ya moja kwa moja inayoweza kumpa mtu nguvu kwa haraka zaidi. Tukumbuke unapokuwa umefunga sukari yako ya mwili inakuwa kwenye kiwango cha chini na hii hupelekea baadhi ya wakati kukosa nguvu na hata uchovu mwingi. Unapata tende kwa haraka nguvu inarudi na kurejea katika hali ya kawaida ndani ya muda mfupi.

Ushauri ni kwamba, kuzaliwa kwenye mitende Nabii Issa (AS) na matumizi ya tende kwa Mtume Mtukufu Muhammad (SAW) kuwe ni kipimo cha kujua hekima na faida yake na tupende kuitumia pale inapopatikana.

# Ziara ya Kufana ya Amir Sahib Tabora na Kigoma

*Kutoka uk. 1*

wanajamaat kuwa na mfungamano mkubwa na Ukhalifa kwani hilo ndio tegemeo pekee linalomuwezesha binadamu kutimiza majukumu yake mawili ambayo ni kutoa haki ya Allah na haki za binadamu. Akiwa Tabora aliweza pia kuwatembelea wanajamaat wa Itundu, Kasisi ambapo alifungua msikiti, Urambo alifungua nyumba ya mwalimu, Igoko nako alifungua msikiti na nyumba ya mwalimu. Amir sahib alikutana nao kwa furaha kubwa wanajamaat wa Ibili na Ulyankulu. Ulyankulu sasa kuna msikiti mzuri ambao aliufungua Amir sahib. Wanajamaat na wenyeji wa mji huo walihudhuria sherehe hiyo.

Kutoka Tabora Amir sahib aliingia mkoa wa Kigoma ambao una historia ya kusisimua. Ni katika mkoa huo ndipo wanapotoka Chifu Mohammed Kalufya – mpigania uhuru wa nchi hii, Sheikh Kaluta Amri Abedi – Meya wa kwanza



*Amir sahib, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akiongea na wanajamaat wa Kasisi*

Mwafrika wa jiji la Dar es salaam, Bwana Bakari Rashid Kazema – ambaye kalamu yake haikukaukiwa wino na anakumbukwa kwa kitabu chake maarufu – ***Mambo***, Hemedi Feruzi Mbyana – mfasiri wa ***Mwito Kwa Mfalme Muislamu*** na mwandishi wa kitabu cha ***Ndoa Ya Kiislam*** na Khamis Mbambwa – mshairi maarufu wa Kiswahili.

Kituo cha kwanza cha msafara wa Amir sahib kilikuwani Nguruka ambapo Amir sahib alipokewa kwa furaha kubwa na bashasha kubwa wakiongozwa na bwana Moshi Mohammed Mlekyakule – mwanasiasa mashuhuri wa Nguruka. Mungu Bariki walikuwa na Jalsa Salana na Amir akashiriki pamoja na



*Naib Amir Tabligh na Tarbiyyat akiwaelekeza jambo wanajamaat wa Dodoma*

mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Uvinza. Amir alisomewa shairi la makaribisho na kupewa zawadi ya fimbo ya mpingo. Kutoka Nguruka walipitia Uvinza walikoonana na Mkuu wa Wilaya ya Uvinza aliyewapokea kwa heshima kubwa. Wakiwa Uvinza, Naib Amir alionana na mwanae Chifu Mohamedi Kalufya ambaye anamiliki kituo cha redio.

Mjini Kigoma shughuli zilikuwa nyingi, Amir alionyeshwa kiwanja cha Jamaat kisichopungua ekari kumi. Amir alifurahi sana na akaahidi kuchukua hatua za kukilinda kiwanja hicho.

Amir pia alimtembelea Mkuu wa Wilaya ya Kigoma ambaye aliupokea ujumbe wa Jamaat kwa furaha. Mwishoni Amir sahib alitembelea sehemu za vivutio kwa watalii pakiwemo pale mvumbuzi Henry Morton Stanley, Mwandishi wa Habari Mmarekani alipokutana na Dr David Livingstone na hifadhi za taifa za Gombe maarufu kwa Sokwe ambao wanapatikana mahali pachache duniani.

Katika safari hii Amir sahib alifuatana na Naib Amir anayeshughulika na Mahubri na Tarbiyyat, Sheikh Bakri Kaluta. Sheikh Bakri alitumia fursa hiyo kuwaelezea wanajamaat majukumu aliyopewa na Khalifatul Masih V, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. na akatoa mwito kwa wanajamaat washiriki kikamilifu katika kutimiza matakwa ya Khalifatul Masih a.t.b.a.

## TANGAZO LA IJTIMAA YA 29 YA KHUDDAM-UL-AHMADIYYA TANZANIA

**Tanzim ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania inapenda kuwataarifu Khuddam na Atfal wote nchini kuwa Ijtimaa yao ya 29 itakuwa tarehe 22 - 24 Juni, 2018 Kitonga, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam.**

**In-Shaa-Allah.**

**Khuddam na Atfal wote wanaombwa kuhudhuria bila kukosa.**

***Limetolewa na Idara ya Ish'aat ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania***

## Awa Katibu Mkuu CCM



*Katibu Mkuu mpya CCM Dkt. Bashiru Ally akipongezwa na Mwenyekiti wa Taifa Dkt. John Pombe Magufuli mara baada ya uteuzi wake kutangazwa*

Daktari wa Sayansi ya Siasa Chuo Kikuu Cha Dar es salaam, Bashir Ally amechaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM akichukua nafasi ya Abdulrahman Kinana ambaye amekuwa katika medani za uongozi kwa takriban miaka 40. Daktari Bashir Ally ana sifa ya kujenga hoja bila kupayuka na ni mchapa kazi mahiri. Umakini wake umedhihirika alivyokamilisha jukumu la kuongoza tume ya CCM iliyochunguza juu ya mali za CCM. Kazi hii ameifanya kwa bidii na uaminifu mkubwa. Vyanzo vya kuaminika vimethibitisha kuwa hiyo ilikuwa turufu muhimu katika kuipata nafasi hiyo ya kutumikia chama kikongwe nchini CCM. Licha ya kuwa na mapenzi makubwa ya kusoma vitabu, yeye ni mshairi na anafahamika kama Malenga wa Kavazi la Mwalimu Nyerere.




1. Mzee Daimu Ali Mambo wa Likokona jamaat. Amefariki akiwa na umri wa miaka 76 tarehe 21 mwezi Mei 2018.
2. Mzee Seif Sungu wa Kazole amefariki mwezi 28 Mei 2018
3. Bwana Isihaka Mchawi amefariki tarehe 29 Mei 2018.

*Inna Lillahi wainna Ilaihi rajiuun*

## Utumiaji Simu Wakati wa Itikaf

Imefahamika ya kwamba baadhi ya Mu'takifun hutumia simu wakiwa katika Itikafu mwezi wa Ramadhan.

Vitendo hivi viliripotiwa kwa Huzur Anwar a.t.b.a. ambaye



ameelekeza kwamba:

**"Simu zinatakiwa kuzimwa wakati wa Itikafu. Hakuna haja ya kujiingiza katika shughuli yoyote au mawasiliano binafsi. Kama vinginevyo, dharura inatokea na mawasiliano yanalazimika, mhusika anapaswa kuyafanya nje ya msikiti."**

# Jibu Kwa Sheikh Sawafi - Muibadhi Wa Nchini Oman

Majibu ya Makala iliyoandikwa na Sheikh H. Sawafi Muibadhi wa nchini Oman. Nukta zilizopo katika Makala hii yenye kurasa 18. Japo kuna mambo amerudia yaleyale. Sheikh Sawafi amesema:

**1** Mitume huifadhiwa na Allah kwa hifadhi maalum. Hilo ni kweli.

Lakini hilo ameshindwa kulithibitisha kwa Seyidna Ahmad (as) kama hakuhifadhiwa na kwa hifadhi maalum.

**2** Anasema Mitume wanakuwa ni waaminifu. Hilo ni kweli.

Hapo akamtuhumu Seyidna Ahmad (as) kuwa alishindwa kutunza amana ya wazazi wake akarejea kitabu kinachoitwa ***Siirat Mahd*** cha Khalifa wa pili katika riwaya ya 49 InshaAllah hiyo nukuu tutatafuta na kuiwakilisha baadaye. Wakati tunasubiri usahihi wa tuhuma yake nami ninampatia aya ya Qur`an aitakafari kisha aniletee majibu sawa na tafakari yake. [" Wakasema: kama amekwiba, basi ndugu yake pia alikwiba zamani. Lakini Yusufu akayasiri moyoni mwake wala hakuwadhihirishia. Akasema Ninyi mna hali mbaya; na Mwenyezi Mungu Anajua mnayoyasema"] 12:78 wapo wafasiri wa Qur`an waliosema katika aya hii (12:78) kuwa Nabii Yusufu (as) aliwahi kuiba vitu vichache nyumbani kwa shangazi yake. Je hilo Sheikh sawafi una maoni gani ?

**3** Amesema Mitume wanakuwa ni wakweli. Hilo ni kweli. Akatoa tuhuma juu ya umri wa Seyidna Ahmad (as). Hilo lilishajibiwa maranyingi na angekuwa na hoja katika hilo angetuhumu kupitia majibu yetu lakini kwakuwa hanahoja akaona apige makelele. Kwahiyo nitaweka majibu hayo ambayo yalishajibiwa tayari.

**4** Pia akasema kuwa Mtume hawezi kusema uwongo. Hilo ni kweli. Hapo akatuhumu jambo lilelile lililomo katika ufunuo unaohusu suala la umri wa Seyidna Ahmad (as). Hilo pia lilishajibiwa.

**5** Analalamika kutumia nukuu za Biblia katika baadhi ya mambo na akasema eti Ahmadiya ni mti uliopandwa na kanisa kwasababu ya kuinukuu Biblia katika baadhi ya mambo". Hapo ndipo nilipojiuliza hivi huyu ni Sheikh au? Lakini nilipokumbuka kuwa hata sala ya Ijumaa kaanza kuisali 1970 nikajua huyu inahitaji kuhurumiwa zaidi maana ayasemayo hayajui. Maana ndani ya Qur`an zimo aya nyingi tu zenye maneno yaleyale yaliyomo katika Biblia sasa sijui yeye Qur`an anaichukuliaje ni mti uliopandwa na kanisa? Pia wapo wafasiri wa Qur`an wengi walionukuu Biblia. Sasa sijui na wenyewe ni mti uliopandwa na kanisa?? Ebu Sheikh Sawafi tueleze Biblia sio hoja kivipi?

Je uliwahi kutuuliza swali lolote tukakujibu kwa ushahidi wa nukuu ya Biblia?? Pia mtu msomi anawajibika kujibu hoja sawasawa na hoja ilivyo. Sio kuanza kukwepa hoja kwa kisingizio cha marejeo.

**6** Kichekesho kingine, Sheikh Sawafi amesema kuwa eti aya (69:45-47) inawahusu wadai Utume wa kweli eti haiwahusu wadai Utume wa uwongo. Alafu anasema eti tumpatie aya inayosema mtume muongo anauawa". Hiki ni kituko cha mtu aitwaye Sheikh. Ngoja nimjibu kwa njia ya maswali huenda akazunduka. Kwanza je yupo mtume wa Allah yeyote anayeweza kuzua uongo??. Jibu ni hakuna na haiwezekani mtume yeyote wa Allah kuzua uongo. Au tujaalie amekuwepo mtume wa ukweli kama ufahamu wako ulivyo lakini katika funuo zake akazua uongo na Allah akamuua sawa na aya hiyo kwa kosa hilo je huyo aliye uawa kwa kosa la kuzua uongo ni nani tena atakaeendelea kumuita kua ni mtume wa kweli wakati Allah ameshaamua kwa kosa la kuzua uongo? Jibu lake huyo atahesabika kuwa wa uongo ndio maana Allah akaamua. Pia Sheikh Sawafi mwenyewe amekiri kuwa Mitume huwa wanahifadhiwakwa hifadhi maalumu ya Allah. Sasa iweje Mtume alieyehifadhiwa kwa hifadhi maalumu atie uongo katika funuo zake anazopokea kutoka kwa Allah.

Kwa neno zima Mitume wa Allah hawawezi kuzua uongo wowote katika funuo zao. Na wakizua wanauawa kwa kosa la uongo na wakishauawa wanahesabika ni Mitume wa uongo ndio maana tunasema kuwa aya hiyo ipo kwa ajili ya kupambanua baina ya Mtume mkweli na Mtume muongo. Kwa aya anayouliza Sheikh Sawafi inayosema Mtume wa uongo anauliwa ndiyo hiyo hiyo (69:45-46), pia jambo hilo limeelezwa na wafasiri wa Quran wengi. Na hilo liko wazi hata katika maandiko ya kabla ya Quran.

Nukta ya 7 katika Uk. 5 Sheikh Sawafi amenilisha maneno kinywani kama ilivyo desturi ya maadui wa haki "*jasiri haachi asili*". Amesema eti mimi nimesema kuwa, "wadai Utume wa uongo wanauawa mara moja". Sasa kama mimi nimesema hivyo imekuwaje tena msingi wa hoja yangu ukagota katika kigezo cha muda wa miaka 23? Je, Musallama Kadhaabu aliuawa siku ile ile aliyodai Utume? Na kigezo cha miaka 23 sikukiweka mimi wala hakikuwekwa na Seyidna Ahmad a.s bali kilikuwepo miaka mingi kabla ya kuzaliwa kwa Seyyidna Ahmad a.s, swali tunalowauliza wapinzani wa haki na siku zote huwa ni mwiba kwao. Watuletee mfano katika historia ya dunia je, kuna mtu yeyote aliyewahi kudai Utume kisha akaishi miaka 23 baada ya kutangaza funuo zake amefunuliwa na Allah? Mpaka leo hajawahi kumpata na hatompata na hilo linathibitisha kuwa kipimo cha miaka 23 ni kipimo cha haki na wanaokikataa ni hawa wapinzani wa Seyyidna Ahmad a.s na kinachowafanya wakikatae ni kwa sababu Utume wake ulidumu kwa miaka 26. Na wote wanaokipinga wanakipinga kwa inadi, husda na khiyana.

Nukta ya 8 katika Uk. 6 "Sheikh Sawafi amenilaumu eti nimeacha kunukuu aya zinazozungumzia Mitume wanaomzulia Allah uongo badala yake nimenukuu aya zinazozungumzia Mitume wa haki". Hii ni ajabu ya huyu mtu aitwae sheikh. Mimi ninadai kuwa Seyidna Ahmad a.s ni Mtume alafu anataka eti nithibitishe



**Ahmad Abdul Bishazo**

ukweli wake kwa kunukuu aya za watu waongo. Kwa taarifa yako kazi hiyo sio yangu bali ni ya kwako wewe ulie adui wa haki, maana watu wa kweli hufana. Hivyo ni haki kuthibitisha mtu mkweli ndani ya watu wakweli kwa dalili. Na Sheikh Sawafi anayo haki ya kuthibitisha mtu muongo ndani ya waongo kwa dalili zinazotolewa. Na hapo ndipo ulitakiwa kukumbuka swali nililokuuliza ambalo hukulijibu kabisa nalo ni hili; Wakristo wanaamini kuwa Yesu ni Alfa na Omega na wanasema kuwa Mtume S.A.W. sio Mtume wa kweli na hakutumwa na Mungu na hajatajwa popote katika vitabu vyao. Nikakuuliza, Je wewe Sheikh Sawafi unatumia kigezo kipi kuwathibitishia Wakristo kuwa Mtume S.A.W. ni mtume wa kweli? Mpaka sasa kimya. Nukta ya 8 uk. 6

8. Sheikh Sawafi amepinga eti "kukatwa mshipa wa shingo(69:45) sio kuuawa kwa kudai Unabii wa uongo". Huyu Sheikh anapinga bila dalili yoyote, nimkumbushe tena. Manabii wa uongo wapo duniani karne na karne mpaka sasa.Tuletee walau mtu mmoja tu ambaye aliwahi kudai kuwa yeye amepokea funuo na akatangaza kuwa ni Nabii kisha Allah akamuacha hai kwa kwa muda wa miaka 23. Pia maana aliyoikubali yeye kuwa ndio maana sahihi ya "kukatwa mshipa wa shingo" amesema kuwa ni "kudhalilishwa" kwa madai Utume wa uongo hilo ni sawa lakini halivunji ahadi ya Allah kuuawa kwa Mitume waongo. Pia Sheikh Sawafi amesema kuwa, Seyidna Ahmad a.s. lidhalilishwa na Allah kwa hiyo maana ya kukatwa mshipa wa shingo ilitimia kwake. Hiyo ndio ajabu ya huyu mtu aitwae Sheikh Sawafi. Kule mwanzo katika Makala hii alisema kuwa aya (69:45-46) hairuhusu kumuingiza mdai Unabii wa uongo bali inawahusu Mitume wa haki tu. Na akanitahadharisha kabisa kuwa aya hizo hazimuhusu Seyidna Ahmad a.s lakini hapa amekubali kuitumia hiyo aya katika kumpinga Seyidna Ahmad A.S. Wakati alishakataa katakata aya (69:45-46) hiyo kuihusisha na Seyidna Ahmad a.s, hilo ndilo tatizo la husuda, hiyana na inadi. Hapo ndipo tunajuwa kuwa kule juu amepinga ilimradi tu asikubali haki ambayo ameshaijua. Pia tukienda katika uhalisia wa kutaka kujua kama Seyidna Ahmad (as) alidhalilishwa kama anavyodai Sheikh Sawafi.

Njia rahisi ya kujua udhalilishaji wa mtu unatakiwa umpime kwa kumlinganisha na maadui zake katika kila hali maana katika uadui ni rahisi kujua upande upi unaopata msaada wa Allah. Kwa sababu Allah daima Anawasaidia wakweli. Leo hii ukiwachunguza walio ni maadui wa Mtume (s.a.w) utapata jibu. Sasa Sheikh Sawafi jaribu kusoma historia ya wapinzani wa Seyidna Ahmad (as) watu kama Sheikh Muhammad Hussen wa Batala n.k ujue hao mwisho wao ni upi? Na nini walichokiacha nyuma yao? Utapata kujua ni nani aliyepata kudhalilishwa na Allah na nani aliyehifadhiwa na Allah katika hifadhi maalum.

Nukta ya 9 uk. 7 Sheikh Sawafi amekiri nukuu tulizoziweka za wanachuoni zinaeleza uwepo wa kipimo cha miaka 23 ya kupambanua Mtume wa kweli na Mtume wa uwongo. Lakini Sheikh Sawafi amewakosoa wana chuoni hao kuwa waliteleza. Kwanza nimfahamishe kuwa wanachuoni waliosema hayo ni wengi mno na hapo tuliwanukuu wachache. Pia Sheikh Sawafi amekataa bila dalili yeyote. Sasa Shekh Sawafi zipo njia za kuwakosoa wanachuoni je huzijui? Nafupisha maneno. Sheikh Sawafi nakuomba uniletee mwanachuoni yoyote ambaye amewahi kupinga kipimo cha miaka 23. Sharti uniletee mwanachuoni wa kuanzia mwaka 1835 kurudi nyuma. Usiniletee mwanachuoni wa baada ya hapo.

Nukta ya 10 uk. 11 Sheikh Sawafi amesema kuwa aya 7:95. Inahusu Mitume kabla ya Mtume (saw) aya yenyewe ni hii. "Na Hatukumtuma Nabii yeyote katika mji wowote isipokuwa Tuliwashika wenyeji wake kwa taabu na mashaka iliwapate kunyenyekea". Hapa ufinyo wa fahamu yake umedhihirika waziwazi Kwanza ni kuuliza je waliompinga Mtume s.a.w. hawakuadhibiwa na Allah? Na kama waliadhibiwa unawezaje kumtoa Mtume (saw) katika aya hii 7:95? Kusoma haujui hata picha huoni jamani. Nimfahamishe huyu aitwae Sheikh Sawafi kua Manabii ni ndugu na wanazo sifa zinazo fanana na kupitia hizo huwa rahisi kuwatambua kwa hiyo sifa yeyote ambayo Allah Ameiegemeza kwa Manabii wote basi hiyo kila Nabii awe nayo na kama hana basi huyo si Nabii wa kweli. Mfano Aya hii " Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hakuna aabudiwaye ila mimi, basi niabuduni." (21:26) Je muundo wa Aya hiyo (21:26) unaweza kuutofautisha na muundo wa Aya ya (7:95) anayopinga Sheikh Sawafi. Je hapo unaweza kusema hilo haliwahusu Mitume wote waliopita, waliopo na wajao na ukweli ni huu asiyekuwa na sifa hiyo huyo sio Mtume wa Allah. Aya za namna hiyo zipo nyingi na ndizo haswa Sheikh Sawafi anazotakiwa kuzitumia katika kumpinga Seyidna Ahmad (as).

Nukta ya uk. 12-13 Sheikh Sawafi haeleweki anasema nini, malalamiko si malalamiko na hoja si hoja. Lakini kuhusiana na balaa la ugonjwa wa tauni, InshaAllah nitaileta nukuu kutoka katika kitabu cha ***Kinga Ya Balaa*** na yeyote anaweza kujisomea kitabu hicho maana Seyidna Ahmad as mwenyewe amejibu upinzani wote unaohusu ugonjwa wa tauni.

Nukta ya 13. Uk ,16-18. Sheikh Sawafi ametutuhumu eti sisi Ahmadiyya ni waongo wa kutoa takwimu za wanajumuiyya. Hapa nimjibu kwa ufupi tu. Yeye Sheikh Sawafi ameweza kuleta hoja inayo onyesha idadi inapanda na kupungua. Kama tungekuwa waongo kama anavyosema tusingekuwa tunatoa takwimu zenye kuonyesha kupanda na kushuka bali tungekuwa tunatoa takwimu zenye kupanda tu. Pia Sheikh Sawafi anatakiwa kuelewa Sensa hiyo tunaifanya sisi wenyewe sasa ni nani anayegundua uwongo wetu wakati sensa tunafanya wenyewe kwa njia tuzijuazo. Labda kama mngetufanyia sensa nyinyi kisha mkawapa idadi iliyo tofauti na ya kwetu hapo ningemtuhumu kuwa sisi ni waongo. Pia muelewe kama watu wanahesabu pesa wanakosea sembuse idadi ya watu. Pia muelewe wanafanya kosa la takwimu katika Jumuiyya katika mazingira ya uzembe au ndio uovu huwa wanachukuliwa hatua sasa mnawezaje kushikilia jambo hili kama hoja ya kuthibitisha ukweli wa Ahmadiyya.

Mwisho. Je Ibadhi mpo wangapi duniani? Je Sunni ni wangapi duniani? Je Shia ni wangapi duniani? Kama hamna majibu ya maswali hayo basi mjue kazi hiyo sio ndogo ndio maana nyie imewashinda kabisa.

# Bustani ya Washairi

### UCHAMUNGU

Uchamungu ni daraja,tena daraja la shani
La kuipata faraja, na kwenda hadi peponi,
Pepo ndio tafurija, kwa wale waloamini,
Uchamungu ndiyo njia, ya kujivusha ng'amboni

Bila kuwa mchamungu, huwezi pata auni,
Ya kukwepa ulimwengu, na kumpata Manani,
Katu tusimwache Mungu, kumfuata shetani,
Uchamungu ndiyo nuru, imulikayo gizani,

Wachamungu watapewa, haki zao kwa Manani,
Siku ya kuhesabiwa, kwa wote wa duniani,
Na hicho ndicho kipawa, kwa wale waja makini,
Uchamungu ndiyo njia, ya kujivusha ng'amboni

Ninamaliza kutunga, shairi la uchamungu,
Kudhukuru mwenye mwanga, muumba wa ulimwengu,
Kwani yeye kaijenga, Akhera na ulimwengu,
Uchamungu ndiyo nuru, imulikayo gizani

**Zaid Abdallah Machombe**
**Ni mwanafunzi wa kidato cha II**
**Shule ya Sekondari Mabibo**



### KWA NINI IWE HAPANA!

Bisimilahi naanza, Kwa hili ninalonena,
Nataka kuwauliza, kwa nini mnaukana,
Ukhalifa wa Muweza, uloletwa kutupona,
Kwa nini iwe hapana, ikiwa nyie hamna?

Kwa fadhila za Msuza, Allah ametujaliza,
Karne kuimaliza, na minane kuongeza,
Watano kutuongoza, Khalifa wake muweza.
Kwa nini iwe hapana, ikiwa nyie hamna?

Mulibuni kwa dakika, mara mkatokomea,
Wetu sisi wa miaka, dunia yashuhudia,
Tuwapata kwa baraka, kutoka kwake jalia,
Kwa nini iwe hapana, ikiwa nyie hamna?

Kiongozi waumini, kitabu chake manani,
Chawabana kibanoni, kuwauliza kwanini,
Mwaipinga Qurani, dhidi ya hili jamani,
Kwa nini iwe hapana, ikiwa nyie hamna?

Aya zimefululiza, kutoka kwake Latwifa,
Ila moja tosheleza, kutambua Ukhalifa
Lakini bado mwazoza, kuupinga siyo sifa,
Kwa nini iwe hapana, ikiwa nyie hamna?

Suratul annura, tano sita yaeleza,
Walofanya yalo bora, kweli atawajaliza,
Hamkupewa sitara, swali hili nauliza,
Kwa nini iwe hapana, ikiwa nyie hamna?

Khalifa atatokea, toka miongoni mwetu,
Kuja kutufunza njia, kumpata mola wetu,
Kwa kufata manabia, enzi ya kizazi chetu,
Kwa nini iwe hapana, ikiwa nyie hamna?

Anopinga Qurani, basi huitwa kafiri,
Mtanieleza nini, kunijibu bila shari,
Ikiwa ni Qurani, inathibitisha ya heri,
Kwa nini iwe hapana, ikiwa nyie hamna?

Ninawaaga kwa heri, wale wanao ukana,
Nitungieni shairi, kunieleza bayana,
Kwa nini mwaukana, ukweli waonekana,
Kwa nini iwe hapana, ikiwa nyie hamna?

**Zaid Abdallah Machombe**

### NYAMA WAFUGWA NA WATU

Shairi fanya hisani,waendee ndugu zetu
Nina hadithi yakini, ifike kwa wanakwetu
Palikuwa sulutani, alifuga mbwa mwitu
Nyama wafugwa na watu, huwadharau wenzao

Alifuga wengi sana, mfano kama vimatu
Usiku hata mchana, uwanja hupiti katu
Sheti mtatafutana, wawili au watatu
Nyama wafugwa na watu, huwadharau wenzao

Huwalipia gharama, akawapa kila kitu
Nyumba mchele na nyama, kofia hata viatu
Basi huwa na vilema, wakasahau msitu
Nyama wafugwa na watu, huwadharau wenzao

Haja yake kuwatuma, walinde wezi na chatu
Wasipitishe dhuluma, na kuharibu vya watu
Wawe tumbiri na kima, wakawatia supatu
Nyama wafugwa na watu, huwadharau wenzao

Siku moja sulutani, alitembea na faru
Kakuta swala na nyani, wasema kwenye fukutu
Mbwa kavunja hisani, kawa kama si mwenzetu
Nyama wafugwa na watu, huwadharau wenzao

Heshi kututia dhiki, kwa kujivutia utu
Tuendako hatufiki, vidole huwa mabutu
Tupatacho hakiliki, vinywa vimejaa kutu
Nyama wafugwa na watu, huwadharau wenzao

M-mbwa hutuki unyama, kwamba wafugwa na watu,
Lakini dumu daima, upunguze utukutu
Au sivyo utakwama, hapo utapothubutu
Nyama wafugwa na watu, huwadharau wenzao

**Sihiyana Saleh Mandevu *(Mtenda Mema)***

### USIKU HUWA MCHANA

Leo chereko chereko, Mandevu najikokota
Nimesikia kicheko, cha hasini na cha sita
Mtu chake bado yuko, Dola amezikamata
Usiku huwa mchana, Ya leo hushinda jana

Bwana ninakupa heko, bila ya kusitasita
Kwa yale maneno yako, matamu kama kashata
Kupanda shamba si lako, mtu kweli utajuta
Usiku huwa mchana, Ya leo hushinda jana

Zamani mimi mwambao, yaliwahi kunikuta
Shambani kwa mfamao, niliupanda ufuta
Yalipofika mazao, hata chembe sikupata
Usiku huwa mchana, Ya leo hushinda jana

Basi siri ya mtungi, sana ajuwae kata
Watu wengi hatukingi, japo tukienda peta
Ukivaa hudhurungi, watu hukuona sura
Usiku huwa mchana, Ya leo hushinda jana

Mtu kutega ndowano, kwanza ukachimbe mvata
Ukileta majivuno, kambale hutompata
Ukali wa msumeno, umeshindwa kwenye nta
Usiku huwa mchana, Ya leo hushinda jana

Sasa hizo taarifa, naipiga tarumbeta
Usipo uziba ufa, hasara itakupata
Utapatwa na maafa, ya kuujenga ukuta
Usiku huwa mchana, Ya leo hushinda jana

Yote uliyoyanena, yamekuwa tabilita
Wengi waliojivuna, siku hizi wametota
Mfano kama watwana, wanabeba malobota
Usiku huwa mchana, Ya leo hushinda jana

Wako wapi mafusuli, waliokuwa wakinata
Sheria hawakubali, wakiamini matata
Sasa hawana kauli, mfano wa mazezeta
Usiku huwa mchana, Ya leo hushinda jana

**Sihiyana Saleh Mandevu *(Mtenda Mema)***

### 'KUBETI' SIO IBADA

Fikira tumezizika, kubaki na visirani
Na ubongo umelika, Umepukuswa kiini
Mchwa sasa unacheka, kajivisha udoni
Mjumbe akishafika awajuze ya kisiwani

Ujumbe mtaushika, msipoafiki tupeni
Lawama nisilka, tumerithi uhengani
Hatutaweza pilika, umbea mitandaoni
Mjumbe akishafika awajuze ya kisiwani

Kisiwa kimelipuka, na ugeni wa uzunguni
Tunavijaza viduka, kalamu mkononi
Tunaita mikeka, karatasi za uchinani
Mjumbe akishafika awajuze ya kisiwani

Kigezo ni soka, wakapitisha sheriani
Chenji zatutoka, kutamani mamilioni
twatoa sadaka, isohalalishwa na dini
Mjumbe akishafika awajuze ya kisiwani

Hatutaki chakalika, kutwa magengeni
Tumbo zimechoka, shibe kwa mgeni
Miguu yapauka, pekupeku barabarani
Mjumbe akishafika awajuze ya kisiwani

**Daudi Mkuty (*Simba*)**

### NALILIA FIMBO YANGU

Fimbo yangu ya mpingo, imekatika taani
Imeharibu mpango, kutwa nimo mashakani
Navurugika ubongo, nikenda macho sioni
Yailahi ya Manani Nalilia fimbo yangu

Miti hii ya mipingo, sasa haipatikani
Si kama ile mikongo, iko mingi misituni
Ningechonga hata gongo, nikashika mkononi
Yailahi ya Manani Nalilia fimbo yangu

Tazama hivyo vioja, uwezo wake manani
Mikwaju na mikongoja, iko tele magengeni
Hii kwangu iko moja, si nyingi barabarani
Yailahi ya Manani Nalilia fimbo yangu

Imechongwa kwa malengo, nao uzuri wa shani
Umbile la mviringo, hutiwa pembe mwishoni
Basi hufanya maringo, nirandapo mtaani
Yailahi ya Manani Nalilia fimbo yangu

Mola Mjuzi wa yote, mjuzi wa kila fani
Nashindwa kumeza mate, usingizi kwangu duni
Nipe kitu nipakate, inipungue huzuni
Yailahi ya Manani Nalilia fimbo yangu

Fimbo hiyo naisifu, ina uzuri wa shani
Si fupi wala si ndefu, iko kwenye wasitani
Nyinginezo maradufu, kuziona sitamani
Yailahi ya Manani Nalilia fimbo yangu

Fimbo nitaililia, asubuhi na jioni
Miguu imetatia, nikenda kwenda pembeni
Fimbo hunisaidia, nisikanyage majani
Yailahi ya Manani Nalilia fimbo yangu

Fimbo haikuvunjika, kisa ninawaambeni
Si kama sikuishika, nakataa abadani
Ila imeniponyoka, ikapiga aridhini
Yailahi ya Manani Nalilia fimbo yangu

Leo nafunga kikao, ndugu zangu kwaherini
Wa bara na wa mwambao, na dua niombeeni
Mwenzenu kila uchao, mikono iko kichwani
Yailahi ya Manani Nalilia fimbo yangu

**Sihiyana Salehe Mandevu** (***Mtenda Mema***)

# Je Wajua?

## Kwa nini tunaisoma Qur'an kwa Kiarabu japo hatuelewi?

( Pitia kisa hiki cha kusisimua! )

Mzee mmoja wa Kiislam alikuwa anaishi shambani mashariki mwa kijiji kimoja chenye milima na mjukuu wake. Babu huamka mapema sana kila asubuhi na hukaa kwenye kimeza chake akisoma Quran. Mjukuu wake alitamani kuwa kama yeye na akawa anajaribu kumuiga kila namna alivyokuwa akiweza. Siku moja mjukuu yule aliuliza "Babu! Najaribu kusoma Quran kama wewe lakini siielewi, na ninachokisoma nakisahau punde tu ninapofunga kitabu. Sasa kuna uzuri gani kuisoma Quran?"



Babu kimya kimya akageuka alipokuwa anakoka mkaa na akamjibu, "Chukua kapu hili la mkaa elekea chini kule ziwani nitekee kapu la maji" akafanya kama alivyoambiwa, lakini maji yote yalivuja kabla hajarudi nyumbani. Babu akacheka na kumwambia, "Unatakiwa uchangamke safari ijayo", na akamtuma mjukuu wake tena ziwani na kapu kujaribu tena. Safari hii kijana akakimbia haraka, lakini kapu lilikuwa tupu tena aliporejea nyumbani. Akiwa ameishiwa pumzi, alimwambia babu yake kwamba haikuwezekana kuteka maji kwenye kapu, na akaenda kuchukua ndoo badala yake. Babu akamwambia, :Sitaki ndoo ya maji; Nataka kapu la maji. Haufanyi juhudi ya kutosha tu," kisha akaelekea mlangoni akimtazama kijana akijaribu tena.

Kufikia hapa, kijana alishajua haiwezekani, lakini alitaka kumuonyesha babu yake kwamba hata kama akikimbia haraka awezavyo, maji yanavuja yote kabla ya kufika nyumbani. Kijana akazamisha kapu kwenye ziwa na akakimbia nalo kwa nguvu sana, lakini alipomfikia babu yake kapu lilikuwa tupu tena. Akiwa anatwetwa, akasema, "Unaona babu, ni kazi bure!" "Kwa hiyo unafikiri ni kazi bure?" babu akasema, "Tazama kwenye kapu."

Kijana akatazama kwenye kapu na kwa mara ya kwanza akagundua ya kwamba kapu lilikuwa tofauti. Lilibadilika tokea kapu chafu la mkaa na kuwa safi, nje na ndani.

"Mjukuu wangu, hicho ndicho kinachotokea ukisoma Quran. Unaweza usielewe au kukumbuka kila kitu, lakini unapoisoma, unabadilika, nje na ndani. Hiyo ndiyo kazi (shani) ya Allah s.w. katika maisha yetu."

## CHEMSHA BONGO



**Kwenda Kulia**

1 Khalifa aliyechaguliwa 22 Aprili 2003
6 Mwito wa sala
8 Neno linalojumuisha vitendo vyote katika sala
9 Mwongoza sala
10 Mwezi wa tisa katika kalenda ya Kiislam
13 Masihi Aliyeahidiwa alipata pia lakabu ya "Sultan wa _____"
14 Mwezi wa saba katika kalenda ya Kiislam

**Kwenda Chini**

1 Mji aliozaliwa Mtume s.a.w.
4 Mtume aliyezaliwa 571 A.D.
2 Makao makuu ya Ahmadiyya duniani
3 "Dini ni _____"
5 Maamkiano pindi watu wawili wanapokutana
7 Safari takatifu
11 Mchango wa 1 ya 16
12 Dhamira ya sala

**Majibu Ya Chemsha Bongo la Toleo la Mei :** *Hongereni mliopatia yote*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. AHAD | 8. ILIKI | 15. AZALI | 20. SUNNA |
| 2. HIJA | 9. AMIR | 16. AKILI | 20. SALA |
| 3. ISMAIL | 10. AMANI | 16. AMANA | 21. SANDA |
| 4. KHUDDAM | 11. ASIDI | 17. TANZIM | 22. ASILI |
| 5. SHURA | 12. KAABA | 18. ATFAL | 23. JIHADI |
| 6. TABLIGH | 13. IHRAM | 18. AMINI | |
| 7. DINI | 14. IAAAE | 19. JAMAA | |

## TAFUTA MANENO

Kuna maneno 27 katika jedwali hapa chini. Yatafute 24 yaliyobakia kwa kuyazungushia na Penseli

| | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| W | A | T | H | A | M | U | D | I | J | M | I | Z | T | I | R | Q | N | Q | Y |
| L | G | D | W | G | P | I | F | K | A | B | F | B | V | M | S | L | M | Q | X |
| T | T | L | T | R | T | G | U | W | M | W | T | B | R | I | F | L | K | M | K |
| D | R | M | K | I | X | F | I | A | M | V | B | T | H | P | T | H | A | R | J |
| K | L | B | K | L | I | L | H | O | C | H | R | H | P | K | E | E | K | M | R |
| T | R | I | Y | L | U | D | I | M | A | N | A | B | I | I | U | N | N | J | N |
| W | S | J | I | Y | W | N | B | Q | U | I | J | R | V | V | B | M | D | D | Z |
| M | X | D | N | N | I | C | H | G | H | S | X | N | Z | M | A | W | D | A | O |
| R | A | A | V | M | L | N | N | A | G | M | T | V | P | U | D | O | B | T | M |
| S | Y | P | A | M | P | I | R | Z | L | A | W | F | M | H | H | N | D | M | S |
| N | A | A | L | T | B | A | T | C | X | I | K | H | D | A | I | G | V | P | H |
| Y | W | H | W | M | J | M | H | M | T | L | M | K | U | M | R | O | L | Q | U |
| R | N | W | A | A | W | K | P | A | W | X | C | Q | Z | M | I | Z | N | A | K |
| L | C | M | H | B | F | V | B | R | J | U | R | P | U | A | F | O | M | X | U |
| L | M | S | Y | W | A | W | V | D | B | I | J | L | R | D | U | I | K | B | R |
| B | I | N | A | D | A | M | U | M | Z | N | R | I | I | P | T | H | Y | Y | A |
| K | H | I | F | A | D | H | I | T | D | T | L | A | Z | A | Y | Y | X | W | N |
| V | J | T | Z | H | V | U | K | R | I | S | T | O | Y | A | N | D | F | J | I |
| V | H | K | H | A | T | A | M | A | N | N | A | B | I | Y | Y | I | N | V | F |
| H | H | P | V | Y | N | G | K | M | S | A | M | A | H | A | T | C | G | N | N |

# Buriani 'Guru' Wangu Omari B. Bumbo

Na **Mwl Abdullah H. Mbanga** – Mtwara

Omari Bakari Bumbo alikuwa mtu mwenye mtambo wa kimo, mwili wake ulijengeka kwa misuli ya nguvu. Sauti na sura yake vilidhihirisha ubabe ulokuwamo ndani yake, lakini tabia yake ya kuzungumza kwa upole huku akiweka kibwagizo cha "au sivyo eh" kila baada ya sentesi moja au mbili, ilidhihirisha utofauti wake na wababe wa kawaida wa mitaani. Mtu huyu aliyekuwa na shauku kubwa ya kuhubiri ujumbe wa Ahmadiyya popote alipokuwa na aliyekuwa akijiamini mno katika mijadala alifariki dunia mnamo tarehe 15 Aprili 2018 INNA LILLAHI WA INNA ILAIHI RAAJIUUN (Hakika sisi ni wa Allah na hakika Kwake tutarejeshwa)

Mara ya kwanza nilikutana na Omari Bumbo mwaka 1984 nilipokuwa nimehamia Mabibo nikitokea Mburahati Mianzini nilikokuwa nikiishi kabla.

Siku moja nilikuwa nimeketi katika duka moja la vitabu vya Kikristo nilikuwa nikihubiriwa Injili na mhubiri mmoja aliyekuwa na tabia ya upole na upendo wa ajabu. Mhubiri huyo ambaye yumkini ndiye aliyekuwa mmliki wa duka hilo, alikuwa ni rafiki yangu wa karibu mno. Alinivutia kutokana na tabia yake ya kuhubiri upendo na amani, jambo ambalo niliamini kuwa ndio malengo makuu ya kuletwa kwa dini duniani.

Mwinjilisti huyo alikuwa mara nyingi akinipatia vitabu na vipeperushi mbalimbali vilivyokuwa vikinilingania imani ya Kiinjilisti. Kwa kiasi fulani viliniathiri na kunifanya nianze kutamani hata kujiunga na Ukristo. Nilikuwa mshabiki wa hoja tangu utotoni mwangu, hivyo kwa kuwa mhubiri yule alikuwa akiwanyamazisha Waislamu wengi kwa hoja nilitokea kumkubali mno.

Hata siku nilipokutana na Bumbo dukani hapo nilikuwa naendelea kuhubiriwa Injili. Wakati rafiki yangu yule akiwa amenipatia vitabu viwili na vipeperushi kadhaa na akawa ananisisitiza kufuata dini yenye upendo na siyo dini ambayo hata viongozi wake wamejaa hasira na chuki dhidi ya wenzao. Alitamka haya kwa bashasha akiwa anatabasamu kwa ujumla sikuwahi kumuona akighadhibika katika mijadala ya kidini.

Ndipo ghafla siku hiyo, katikati ya mazungumzo yetu akaingia mtu mnene, mrefu, mwenye uso mpana na machache yaliyoniashiria kuwa lazima alikuwa ni Mrufiji na kwa hiyo tutakuwa na uhusiano hata wa kikabila.

Lakini mtu huyu sikuwahi kuonana naye kabla. Alikuwa amevalia fulana yenye kola ambazo vijana wa sasa huziita 'form six' yenye rangi ya kijani kibichi na mistari miyembamba miyeupe ya ngazingazi, akiwa pia amejifunga msuli Kipwani-pwani kabisa, niliamini kuwa haishi mbali sana na eneo hilo.

Hali ilionyesha kana kwamba yule Mwinjilisti na lile bonge la mtu walikuwa na kiporo cha mjadala, hivyo bwana yule alikuja ili wakimalizie. Mhubiri wangu alionyesha hali ya wasiwasi, alionekana kuhaha kumzuia mtu yule 'bwana machale' kama nilivyoamua kumbatiza kimoyomoyo, aliendelea kuhoji juu ya suala la kuchinja.

Nilimsikia akirejea karaa fulani za kutoka katika Biblia kuonyesha kuwa Ibrahim ambaye Wakristo wanadai kuwa ni baba yao wa imani akichinja, hivyo kwa nini wao Wakristo ambao ni wana wa Ibrahim hawaendelezi sunna hii?

Hoja hii ilionekana kumkwaza mno yule 'Mristo wangu' ambaye alionekana kutokuwa na jibu la hoja hii. Alianza kuhamaki, kwa mara ya kwanza nilimshuhudia yule swahibu wangu akipoteza uvumilivu na bashasha aliyo nayo. Alikuwa akimuomba yule bwana aondoke pale dukani maana alikuwa akimletea fujo.

Mtu yule aliyeonekana mwenye kujiamini mno, hakuwezekana kumuondoa kirahisi. Mwinjilisti wangu alianza kubwata kwa hasira akimfukuza yule mpinzani wake ambaye sikuweza kumbaini iwapo alikuwa ni Muislam, Mkristo wa madhehebu pinzani au ni mtu asiye na dini aliyeamua kuwapa changamoto waumini. Niliondoka nikiwa na maswali mengi. Maswali yaliongezeka zaidi kichwani mwangu siku tatu au nne baadaye ambapo nilikumbana tena na bwana yule



*Omari Bakari Bumbo*

kwenye baraza la wacheza bao, ambapo huku akisafiri, kukala kutakata na kulala, alikuwa akiwanyamazisha wale Waislam juu ya hoja ya ujaji wa Nabii Issa mara ya pili. Alikuwa akisema: "Issa hawezi kurudi bwana, maana yule ni Nabii wa banii Israiila, au sivyo eh!" Quran inasema hivyo hivyo "WA RASUULAN ILAA BANII ISRAIILA" (Naye atakuwa Mtume kwa wana wa Israeli 3:50) au sivyo eh! sasa kama huyu atarudi aya hii si itabidi ibadilishwe au iongezwe maneno yasemayo atatumwa na kwa Waislamu pia? Au sivyo eh!"

Alisema haya huku akirusha kete kwa madaha wakati akimtoa mtu 'hamna' katika mchezo wa bao.

Tukio hili likanivuruga zaidi, nikashikwa na mshangao mkubwa juu ya mtu huyu. Siku chache zilizopita nilimshuhudia akimnyamazisha Mwinjilisti, lakini leo namshuhudia akiwasulubu Waislamu kwa hoja kutoka kwenye kitabu chao. Ilibidi niulizie wenyeji juu ya mtu huyu ambappo nilifahamishwa kuwa yule ndiye "Bumbo Kadiani', mtu mwenye uwezo wa kuwakimbiza Waislamu na Wakristo katika ulingo wa hoja.

Nilivutiwa mno na staili yake ya upangaji wa hoja, na namna yake ya kujiamini iliniathiri vilivyo. Niliamua kutafuta ukaribu na mtu huyu, ambapo baadaye ilibainika kwangu huyu alikuwa ndiye Bw. Omari Bakari Bumbo ambaye baada ya mahusiano yetu ya muda mfupi alikuja kugeuka kuwa 'Guru' wangu aliyenionyesha njia ya kuungana na Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Nilihisi nina deni kubwa kwake pale nilipopokea taarifa za kifo chae nikiwa katika mahudhurio ya kikao cha Majlis ya Taifa, jukumu ambalo lilinizuia kushiriki maziko yake kimwili, ingawa kiroho nilikuwa mshiriki wa maziko hayo yaliyofanyika Ikwiriri, Rufiji.

Omari Bakari Bumbo alizaliwa katika kijiji cha Kibiyo tarafa ya Ikwiriri wilayani Rufiji mkoa wa Pwani.

Hakuwa akikumbuka tarehe ya uzawa wake, lakini alikuwa akidai kuwa ilikuwa ni mwishoni mwa vita vya pili vya dunia, baadhi ya watu wake wa karibu wanautaja muda wa uzawa wake kuwa ni mwishoni mwa mwaka 1946 au mwanzoni mwa mwaka 1947. Alizaliwa na jina la Maulidi kabla baadaye kuitwa Omari.

Omari Bumbo hakuwahi kuonja masomo ya shuleni katika utoto wake, bali alipelekwa chuoni kwa masomo ya dini. Mwalimu wake wa kwanza alikuwa ni Sheikh Omary Mtanga ambaye miaka ya baadaye alikuja kujipatia umaarufu kwa kupinga mambo ya bidaa katika Islam. Hata hivyo katika utu uzima wake Bumbo alikuwa ni mtu anayejua kusoma na kuandika.

Akiwa na umri wa takriban miaka 20, Omari Bumbo aliingia jijini Dar es salaam katika harakati zake za utafutaji wa maisha.

Jijini Dar es salaam, Bumbo alijishughulisha na shughuli mbalimbali zikiwemo vibarua na uchuuzi wa biashara ndogondogo, baadaye aligeukia katika fani ya useremala aliyodumu nayo kwa muda mrefu kabla ya kuibukia katika ukandarasi katika siku zake za utu uzima.

Bumbo alikuwa akikumbuka siku zake za ujana zilivyokuwa na changamoto nyingi.

Anasema mara nyingi alijikuta katika mkabala na wababe wa Manzese wakati huo waliokuwa wakikusanya fedha kwa vijana wachuuzi.

Tabia hii ya uonevu ilimkera bw. Omari Bumbo na hivyo hakuwa tayari kuitii. Bumbo kwa kawaida ni mtu mwenye nguvu za mwili kiasili. Hii ni sifa maalum ya familia yao. Hakuwa mgomvi, lakini hakuwa tayari kunyanyaswa, hivyo kila alipofuatwa na wababe wake aliwagomea, hali hii ilipelekea kuzuka kwa mapigano ambapo aghalabu Bumbo aliibuka mshindi.

Baada ya wababe wa Manzaese kuchoshwa na ubishi wa Omari Bumbo, ambaye wakati huo alikuwa bado mgeni wa jiji, na alikuwa akiishi Mabibo na kuamkia Manzese kwa ajili ya shughuli zake za utafutaji, waliamua kumleta mbabe wao mkuu wakati huo alikuwa akiitwa Mwamba Kessy ambaye ilisemekeana kuwa hapigiki.

Hiyo ilikuwa ndiyo siku ambayo Bumbo alianza kuheshimiwa na kuogopwa na wababe wote wa Manzese. Anasimulia kuwa alimtandika Mwamba Kessy vichwa vya mfululizo vyenye kasi ya kushangaza, vilikuwa vichwa kati ya saba au tisa, hakumbuki idadi yake sawasawa.

Hatimaye Mwamba Kessy alianguka mlegevu akiwa hana hamu ya pambano. Kuanzia siku hiyo Omari Bumbo akawa ndiye kimbiliio la wanyonge wote waliokuwa wakinyanyaswa katika eneo la Manzese hadi Mabibo.

Mwanzoni mwa miaka ya 1970, Bumbo alioa mke wa kwanza. Mwaka 1973 alibahatika kupata mtoto wa kwanza ambaye ni binti.

KUIFAHAMU AHMADIYYA

Ni katika wakati huo huo ndipo Bwana Hanif Mpogo na kaka yake Iddi Mpogo walipohamia Mabibo. Baadaye Iddi Mpogo na Omari Bumbo walikuwa wakishirikiana shughuli za useremala, ushirikiano huu ulianza mnamo mwaka 1975. Wakati huo Iddi na Hanif Mpogo walikuwa wameishafanya Baiat kupitia mjomba wao Sheikh Ali Salum Ndendekile.

Bumbo alikuwa imamu msaidizi wa msikiti ulioitwa Masjid Akbar uliokuwa mtaani kwao huko huko Mabibo. Kwa kuwa kwake Imam mara kadhaa alikuwa akikabiliana kwa hoja dhidi ya mshirika wake wa kazi Iddi Athumani Mpogo ambaye wakati huo alikuwa kijana mwenye hamasa kubwa ya kuhubiri. Mabishano yao wakati mwingine yalipelekea kumualika Mzee Ali Salum Ndendekile ambaye alikuwa ni mtu mwenye uelewa mkubwa wa Qur'an Tukufu.

Kadiri mijadala hiyo ilipoendelea Bw. Bumbo aliendela kuelimika. Aliendelea kupoa zaidi alipogundua kuwa mtu kama Hanif Mpogo alibadilika mno kielimu ndani ya muda mfupi tu baada ya kujiunga. Iddi Mpogo pia alionekana kuimarika zaidi katika ufahamu wa Qur'an Tukufu, hatua ambayo ilimstaajabisha na hivyo kuamua kuanza kufuatilia mafundisho ya Ahmadiyya.

Mwenyewe alikuwa akikumbuka kuwa mnamo mwaka 1976, katika maonyesho ya Sabasaba barabara ya Kilwa jijini Dar es salaam ndipo kiu yake ya kuifahamu Jamaat ilipokatika zaidi.

Huko alitembelea banda la Jamaat Ahmadiyya na kukuta Tabligh ya hali ya juu ikiongozwa na Sheikh Jamil Rahman Rafiq.

Aliathirika mno na Jamaat na hatimaye akajiunga. Ilikuwa mwishoni mwa mwaka 1976, na mnamo mwaka 1977 ndipo akawa Ahmadiyya kindakindaki. Omari Bumbo, Iddi Mpogo na Hanifu Mpogo wakawa kero kubwa katika kitongoji chao dhidi ya Masheikh wa Kisunni.

UPINZANI

Kama ilivyo sunna ya Manabii wa Allah kwamba wafuasi wao ni lazima wapate misukosuko kwa ajili ya imani yao, Bumbo pia hakuwa na kago dhidi ya sunna hii.

Mara tu habari zilipozagaa kuwa Bumbo amejiunga na Jamaat, kwanza alivuliwa uimamu katika msikiti aliokuwa akisalisha.

Baadaye akatengwa na marafiki na alikuwa akitukanwa hata na wale waliokuwa maamuma wake. Aghalabu alikuwa akiwajibu kwa upole na adabu. Maadui zake waliona kuwa kujiunga kwake kungeweza kuathiri wengine kwa kuwa alikuwa miongoni mwa viongozi wa msikiti.

Kwa hivi ilitolewa fatwa kuwa Waahmadiyya wote wanaosali katika msikit ule wapigwe marufuku.

Waahmadiyya wote walialikwa kwenye kikao kuambiwa kuwa hawatakiwi kusali katika msikiti huo. Wao walihoji kulikoni; wakaambiwa kuwa hiyo ni amri ya wenye msikiti. Wakatoa ushahidi kuwa msikiti hauna mwenyewe bali ni mali ya Allah na kwamba hairuhusiwi yeyote kufukuzwa au kuzuiwa kwamba asifike msikitini (2:115).

Mtu mmoja akasema kuwa ingawa msikiti ni wa Allah lakini kuna wanaoitunza ambao ni wanadamu, je; wanaweza kuacha hata mbwa wakaingia humo?

Hoja hii ilimfanya Bumbo ahamaki na kuuliza je! Sisi ni mbwa? Watu wote walikaa kimya na kuhisi kwamba aliyetamka maneno haya aliteleza ulimi.

Bumbo aliendelea kufafanua kuwa hata kama hoja ni umiliki au uchangiaji wa ujenzi wao pia walichangia nguvu na fedha katika ujenzi wa msikiti huo.

Hoja hii iliwanyamazisha Masuni wote msikitini mule, walikauka mate kwa kukosa la kujibu, wakapigwa na butwaa kwa kupwelewa na uzito wa hoja hii. Ndipo mjasiri wao mmoja aliyeitwa Jongo alipofunua kinywa chake na kumaka "Ah! Mimi nilisema! Hawa ni wa kutiwa mikwaju tu, kwa hoja hatutawaweza."

Bumbo aliinuka kwa mithili ya kiboko aliyejeruhiwa na akasema; "hilo ndilo nililokuwa nalisubiri, nani kati yenu anayeweza kututia mikwaju ainuke, we Jongo hivi umenisahau au hunifahamu.....?" alitumia muda mrefu akifoka kwa hasira huku Masuni wale kwa kujua uwezo wake wa upambanaji walianza kushikwa na uoga na kuanza kuondoka mmoja baada ya mwingine, na mkutano ule ukaishia kwa staili hii.

Waahmadiyya waliendelea kutumia msikiti ule bila kubughudhiwa walikuwa hawautumii kwa sala za jamaa.

Bumbo alikumbana na wimbi kubwa la upinzani. Baada ya kujiunga na Jamaat Bumbo alibadilika mno, hakuwa yule akiwaadabisha wababe waliotaka kumuonea.

Bali alikuwa na sera mpya ambayo aghalabu alikuwa akiitangaza kwa aya hii IDFA'UU BIL LATII HIYA AHSAN (ondoa ubaya kwa wema).

Maadui zake walipojua hilo, walitumia nafasi hiyo kuja kumshambulia hata nyumbani kwake mbele ya familia yake. Haikuwa kwa hoja bali kwa kashfa chafu na wakati mwingine matusi ya nguoni.

MITIHANI YA KUJITOLEA

Bumbo alikuwa mtu mwenye msimamo thabiti wa kiimani. Alikumbana na mitihani mingi ambayo pengine ingeweza kumteteresha kiimani. Mathalani alifiwa na watoto wake wawili, baina ya mwaka 1983 -1985, mmoja wa kike Hawa na baadaye wa kiume Hafidh.

Ndugu zake wengi waliamini juu ya ushirikina na hivyo kumtaka afanye chochote juu ya matukio hayo, lakini alikuwa mkali sana dhidi ya dhana hiyo na alisisitiza kumtegemea Allah.

Kuna wakati Omari Bumbo alikosa kazi za kandarasi kwa kipindi kirefu mno. Baadhi ya washirika wake wa kikazi walikuwa wakimwendea kumshawishi juu ya 'kuulizia' kuhusiana upatikanaji wa kazi, mara nyingi aliwaondoa kundini mwake watu waliompa ushauri wa aina hii.

Bumbo pia atakumbukwa mno kwa mapenzi yake ya kujitolea katika Jamaat.

Tangu alipojiunga akiwa Khadim hakukosa kushiriki Waqar-i-amal. Alitumika sana kama mlinzi katika mikutano mbalimbali ya Sabasaba katika banda la Jamaat.

Alikuwa akijitolea kushiriki ujenzi wa mabanda wakati wa Jalsa na ikumbukwe kuwa Waqar-i-amal yake kubwa ya mwisho likuwa ni kusimamia ujenzi wa choo kilicho Jalsa Gah huko Kitonga.

Omari Bakari Bumbo kwangu alikuwa zaidi ya ndugu na rafiki, kwani licha ya kuwa alinionyesha ukweli wa Ahmadiyya, lakini pia alikuwa akiniliwaza na kunipa moyo kila mara nilipopatwa na hali ya mitihani na upinzani kwa ajili ya imani yangu.

Kuna wakati alinilea tu kama sehemu ya familia yake hadi watu wa pembeni walidhan kuwa labda tuna udugu wa damu.

Katika bara Hindi mtu atoaye mwelekeo wa kiimani kwa watu huitwa "Guru".

Ndiyo maana nalazimika kusema: Buriani Guru wangu Omari Bakari Bumbo

# Mapenzi ya Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) Kwa Qur'an Tukufu

*Kutoka toleo Lililopita*

Hadhrat Ahmad (as) amelieleza jambo hili wazi wazi jinsi kutakavyokuwa na uvumbuzi na maendeleo ya sayansi na jinsi maendeleo haya yatakavyosonga mbele ndivyo hivyo usahihi, ukweli na ubora wa mafunzo ya Qur'an Tukufu utakavyothibitishwa na kukubaliwa ulimwenguni.

Hadhrat Ahmad (as) alisema; " ....jinsi sayansi na elimu itakavyogunduliwa, ndivyo utukufu na ukuu wa mafundisho ya Qur'an Tukufu utakavyoenea" (Malfoozat Jal. I uk.86). Hapa itafaa kutaja desturi ambayo kila Mwislamu huishika kwa makini sana. Azaliwapo mtoto katika familia ya Kiislam ni lazima kuwa maneno ya Adhana hutamkwa katika sikio lake moja, na maneno ya Iqamaat hutamkwa katika sikio lake la pili. Hekima ya jambo hili haijulikani na wasio Waislam. Hekima yake ni kwamba kukua kwa mtoto kimwili pamoja na maendeleo yake ya kiroho na ukuaji kwa ujumla huanzia tangu mtoto avutapo pumzi ya kwanza. Akijibu lawama za wanafilosofia wa leo na wa kale, Hadhrat Ahmad (as) alisema; "Hata sehemu ndogo ya Qur'an Tukufu kama tone haina wasiwasi wa kushindwa na wanafilosofia wa kale na wa sasa wakijumlishwa pamoja. Qur'an Tukufu ndilo jiwe litakaloponda chochote kitakachoangukia humo, nacho kitasagwa sagwa katika vipande vipande" (Aaeena Kamalati Islam uk.257). Akizungumzia habari za neema, mibaraka na matunda safi ya Qur'an Tukufu Seyidna Ahmad (as) alisema; "Uzoefu wetu na maoni yetu na ya wale walioondoka duniani kabla yetu, hudhihirisha kuwa Qur'an Tukufu humvutia muumini kwa ajili ya nuru yake na sifa zake za kiroho ziung'arishazo moyo na baada ya kumwonyesha dalili nyingi za utukufu, humuunganisha na Mwenyezi Mungu katika uhusiano usioweza kuvunjika hata kwa upanga mkali. Qur'an Tukufu huufungua moyo na kuyaziba mapengo yasiyostahili na kuinyanyua roho kufikia kiwango cha juu cha uhusiano na Mwenyezi Mungu, pia humpa ujuzi wa kila aina usiojulikana. Pia Mwenyezi Mungu Amewapinga wale wote wawapingao wafuasi wa Qur'an Tukufu na kuwahakikishia kuwa Yeye huambatana na mtumishi wake alifuataye neno lake kwa uaminifu" (Chashma-i-Marafat uk.295 / 296).

Vilevile tunapoangalia hali ya mapenzi yake Hadhrat Ahmad (as) kwa Mwenyezi Mungu, tunaona mfano ambao ulimwengu haujapata kuuona baada ya maisha ya Mtume wetu Muhammad (saw). Wakati Hadhrat Ahmad (as) alipewa cheo cha Unabii na Mwenyezi Mungu, Imani ya watu kuhusu uwepo wa Mwenyezi Mungu ilikuwa imetoweka kabisa. Wengi walikuwa wanaelekea kujiunga na wale wasioamini Mungu kabisa. Wakati ule ulikuwa wakati wa giza. Nuru iliyoletwa na Mtume Muhammad (saw) ilipotea na njia za mawasiliano na Mwenyezi Mungu zilisahauliwa. Basi kulikuwa na sehemu ya dunia wamefufuliwa na kwa kumfuata Masihi Aliyeahidiwa mioyo yao inachangamka na mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Lakini bado wapo wengi wasioamini Mungu au kumuamini kwa kiasi kidogo tu. Wapo watu wengine ambao kila wanapotafakari kuwepo kwa ulimwengu hukiri kuwa hapana budi pawepo na mmoja aliyeweza kuumba dude hili la kustaajabisha. Mawazo yao hayawachukui mbali zaidi ya hapo. Kisha wapo wale ambao hufikiria kuwa yupo kiumbe mdhihilifu ambaye ni mshiriki wa Mungu, naye humwita mwana wa Mungu na humshirikisha sifa zote za Mungu. Wapo pia wachongao mawe na vinyago na kuviabudu kama miungu. Husujudu na kunyenyekea mbele ya vinyago hivyo. Na pia wapo wale wanao waabudu hata wanadamu wenzao. Lakini dini ya Kiislam humweleza Mungu kama Mungu Hai Aishiye milele na ni wa milele. Yeye ni Mhifadhi wa ulimwengu. Ni Mtukufu na Mwenye huruma. Yeye ndiye Bwana na Hakimu wa siku hiyo ya hukumu. Kujinyenyekeza mbele yake tu ndio utatufikisha mbinguni. Mungu wa Waislamu hana wenzi. Hufanya alitakalo. Hana mpinzani. Hakuna chochote kinachoweza kuupinga wema na ufanisi wake na hata jani dogo haliwezi kupepea bila amri yake. Mwanadamu angekuwa duni hata kuliko wanyama kama asipomtafuta Mungu na asipopata radhi yake. Wote tunaelewa kwamba zipo njia mbili za kufikia ufaulu wowote. Mojawapo ni uzoefu na uangalizi wetu. Ya pili ni kusikiliza uzoefu wa wengine na mtazamo wao. Hebu tuwaangalie watengeneza madawa. Wakati wao mwingi huutumia kwa kutengeneza madawa na kufanya utafiti wa madawa yaponyayo maradhi mbalimbali. Majaribio yao na uchunguzi huwasaidia kufikia ufaulu fulani. Matokeo yake ni kwamba hutengeneza madawa mengi kwa manufaa ya watu ambayo huuzwa madukani. Kila mtu hununua madawa haya bila ya kufikiria ni nani kashughulikia utoaji wa madawa hayo. Wala hahitaji kuhoji kama dawa hiyo ni sumu au la. Suala hilo linatuhakikishia kuwa yupo aliyempa kipaji na busara ya kumwezesha kufanya utafiti. Ili kupata mibaraka ya Mwenyezi Mungu mtu hapaswi kutafuta wala kufuata elimu za ulimwengu. Mwenyezi Mungu Muweza wa yote, Katoa habari hii njema katika Qur'an Tukufu kwa watumishi wake Anasema; (Sura Ankabuti aya 70); "Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu, kwa yakini Tunawaongoza kwenye njia Zetu." Yeyote ajivikaye joho la uaminifu akiwa mtumishi wake mwaminifu, awe msomi au mbumbumbu akiwa mweusi au mweupe au awe Mwarabu au asiye Mwarabu, hakika ataiona njia ya Mwenyezi Mungu na atakiri kuwepo kwa Mwenyezi Mungu.


Dkt. Iftikhar Ahmad Ayaz

Hadhrat Masihi Maood alitoa ushuhuda kamili usiopingika kusahihisha makosa yahusianayo na jambo hili. Alifanya hivyo katika vitabu na maandishi yake mengi, katika hotuba na mahubiri yake, na halikadhalika katika mazungumzo ya kawaida. Alisahihisha mawazo yote ya upotevu. Hasa maisha yake yote, tangu utotoni hadi ukubwani amekuwa thibitisho halisi la imani aliyokuwa nayo kwa Mwenyezi Mungu. Wakati fulani alipokuwa akizungumza na marafiki na wafuasi wake, mtiririko wa mazungumzo uligeukia kwenye maoni ya wanafilosofia; "Mwanafilosofia afikiriaye kwa makini mambo ya dunia, na ya mbinguni pamoja na mambo mengine, hukuelezea tu kwamba; ni haki kuwe na muumba, lakini mimi ninakuonyesha kiwango cha juu zaidi kutokana na uzoefu na ufahamu wangu na kukwambia kuwa yuko Mungu" (Malfoozat sehemu III uk.14)

Seyidna Ahmad (as) pia husisitiza kwamba ulimwengu mzima na vyote vilivyomo vimeumbwa kutokana na uthibitisho wa kuwepo kwa Mungu. Hata hivyo watu wa ulimwenguni wameshindwa kutambua hili kwa sababu ya giza katika roho zao; katika tenzi zake nyingi Seyidna Ahmad (as) amefafanua sana habari hizi. Katika tenzi moja ya urdu husisitiza jambo hili anasema;

1. Ni jinsi gani chanzo cha nuru ya nuru kilivyo dhahiri, ulimwengu mzima umejifunua kama kioo cha kujitazamia.
2. Jana usiku nalipata mchocheo nilipouona mwezi, kwani katika akisho lake naliuona uzuri wa Mpendwa wangu.
3. Aa, Mpendwa wangu, ni uzuri gani huu uliokuzunguka? Upande wowote tugeukiao tunafunuliwa njia itakayo tuelekeza kwako.
4. Mawimbi yako hufurika kutoka mwako wa jua, na kila nyota huung'arisha uzuri wako.
5. Vitu vyote virembo huutangaza mvuto wako katika uzuri wao na kila ua la bustanini huudhihirisha uzuri wako.
6. Jicho la kufurahisha la kila kitu kipendezacho huonyesha uzuri wako, na kila fundo zuri la nywele za warembo huelekea kwako wewe.

Katika maandiko mengine Hadhrat Ahmad (as) amesema; "Sababu hasa ya juhudi zangu na huruma ni kwamba nimegundua machimbo ya dhahabu na almasi ambamo nimegundua almasi ya hali ya thamani ya juu sana na ambayo naigawa kwa wanadamu wote, kutokana na kito hicho kila mtu duniani atatajirika kuliko tajiri yeyote ulimwenguni hata angekuwa na dhahabu au almasi ya namna yoyote. Je!, hiyo ni almasi gani? Ni Mwenyezi Mungu, Mola wangu – Mungu wa kweli na njia ya kumwona ni kumyakini na kumwamini Yeye na hivyo utafanya kiungo naye na kupata baraka zake za kweli. Haitakuwa haki kwangu kuificha almasi hii baada ya kuipata" (Arbaeen Na.I uk.2/3)

Katika kitabu chake cha Anjam Atham, Hadhrat Masih Maood alisema; "Enyi wapumbavu, mnawezaje kupata amani mnapoabudu mizimu? Mnapata furaha gani mlapo maiti? Njooni niwaelezeni mahali alipo Mungu hai na pia mumtambue Yu nani. Yeye huzungumza na Manabii wote, lakini mara anafikiriwa kuwa hasemi, yupo leo na Waislamu na anasema nao". Hadhrat Ahmad (as) anamalizia maandishi haya; "Mungu huyo huyo Huzungumza hata leo na mtu yeyote apendezwaye nae. Hata leo Huzungumza na yeyote ampendaye" (Anjam Atham uk.344).

Sisi Waahmadiyya tunaelewa kundi kubwa la watu wake kwa waume katika Jumuiyya yetu, hadi leo wanajua kwa njia ya uzoefu Mungu si kiziwi wala si bubu. Hadi leo huzungumza na wale Awatunukiao na Awapendao. Hata leo Huwasikiliza watumishi Wake wamwombao kwa unyenyekevu. Hadhrat Mirza Bashir Ahmad akiandika kuhusu siku za utoto wa Hadhrat Masihi Maood, alisema; "Jambo muhimu kabisa la kwanza na la mwisho ni pendo la Mungu kwani hicho ndicho kiungo halisi kati ya mwanadamu na Muumba wake. Ndilo tarajio kuu katika asili ya mwanadamu. Ungano la kiroho la Hadhrat Masihi Maood (as) na Muumba wake lilianza vya ajabu hata mtu mwenye akili nyingi angeshikwa na bumbuwazi".

"Hadhrat Masihi Maood (as) aliingia katika maisha ya ujana, wakati ambapo mtu hujazwa hamu ya kujilimbikizia raha akizifuata nyayo za kaka yake. Ni wakati huu ambapo baba yake alimtumia ujumbe kwa njia ya Singa singa mmoja tajiri, kwamba mtu fulani aliyesuhubiana sana na baba yake alikuwa na cheo kikubwa katika nchi, kama Hadhrat Ahmad (as) alipenda kupata kazi ya maana hiyo ndiyo ingekuwa nafasi yake. Huyu tajiri alipompa Hadhrat Ahmad (as) ujumbe huo aliongezea kuwa haitakuwa vyema yeye kutokuikubali nafasi hiyo. Hadhrat Ahmad (as) alimjibu bila ya kusita; "Tafadhali kamwambie baba yangu mpendwa asinihangaikie, kwani nimekwishaipata kazi niipendayo kuliko zote". (Seerat al Mahdi sehemu I).

Yule Singasinga hakuweza kuyaamini hayo, lakini karudi kueleza habari hizo kwa baba yake Seyidna Ahmad (as). Yeye kwa kuwa alikuwa mwenye busara alinyamaza kimya. Baadaye alisema; "Kama Ghulam Ahmad anasema kuwa amepata kazi, hakuna sababu ya kuhangaika. Tena baadaye alisema mara kwa mara "Njia aliyoichagua Ghulam Ahmad ni njia halisi na sahihi. Tunajipotezea wakati wetu". Hata hivyo kwa kuwa alikuwa mtu wa busara na baba mpenzi alikuwa na wasiwasi kuhusu maisha ya baadae ya mtoto wake mdogo. Hadhrat Ahmad (as) pia, kwa kuwa alikuwa mwanadamu alishikwa na wasiwasi jinsi atakavyoendesha maisha yake pindi mzee wake atakapofumba macho yake katika usingizi wa milele, Mwenyezi Mungu Alimfariji mtumishi wake ambaye alikata shauri tangu ujanani kuambatana naye yeye peke yake, na ufunuo wake; 'Alaisallahu bikaafin a'bdahu' (Je Mwenyezi Mungu Hatoshei mja wake)

kabla ya kumaliza hotuba yangu ningependa kuisoma dondoo moja nyingine ambayo inaonesha pendo zito sana la Hadhrat Ahmad (as) kwa Mwenyezi Mungu. Na nuru ya pendo lake ni muhimu mno kustawisha mapenzi ya Mwenyezi Mungu katika roho za wale wanaoungana naye na kufuata nyayo zake. Yeye ndiyo Mtume wa siku hizi na mfano kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa ajili yetu na kumfuata yeye ndio ni kupata radhi ya Mola wetu. Mwenyezi Mungu Amesema; "Bila shaka mnao mfano mwema katika Mtume wa Mwenyezi Mungu" (Al-Ahzaab Aya 22).

# Safari Ya Umrah Na Taratibu Zake

Na **Ali R. Mohammed** – Safarini Qatar

*Kutoka toleo Lililopita*

**Makaamu Ibrahiim**

Mara baada ya kukamilisha kuzunguka Kaaba, Hujjaji anayefanya Ibada ya Haji au Umrah, ataelekea katika sehem nyingine inayoitwa Makaamu Ibrahiim. Eneo hili lipo ndani ya ule mzunguko wa Kaaba, hapa husaliwa rakaa mbili za Nafal, kwa kuomba msamaha wa dhambi zetu kwa Allah, na kuomba mwingi zaidi toka kwake Allah ili baada ya kutoka hapa ukafanye yale yanayompendeza yeye, na Atuepushe na yale Yamchukizayo.

Kumtukuza zaidi Allah na kumsalia mtume s.a.w. Katika sala ya Mtume ambamo ndani yake huombwa heri na baraka kama Ambazo Allah alimtunuku Ibrahiim a.s

Ibrahim alisimama mahala hapa, katika maombi mbali ambayo aliomba akiwa amesimama hapa ni pamoja na kumuomba Allah juu ya kubadilisha maisha ya wakaazi wa bonde hili la Makkah ambalo halikuwa na chochote yaani mimea wala maji.. Pale alipomwomba Allah. "Ee Mola wetu ili hawa watu waelewe lengo Lako, kwanza Ifanye mioyo yao ielekee Kwako na Uwaruzuku riziki kutoka kwako na Uinue Mtume kutoka miongoni mwao, ambaye atawasomea maneno Yako na kuwaonya juu ya dhambi na maovu"

Maneno hayo machache yalikuwa na nguvu ya ajabu kwa kufanya mapinduzi makubwa ya kiroho na kimwili..

Neema zote ambazo tunaziona leo hii katika ardhi hii ambayo haikuwa na kitu, imepata utajiri mkubwa wa gesi na mafuta ambavyo ndio muhimili mkuu wa uchumi wa dunia ya sasa.

Ni Dua ya Seyidna Ibrahim ambayo aliiomba akiwa amesimama mahala hapa..

Ujaji wa Mtume Muhammad s.a.w kama Rehema, wakineemeka wote ni matokeo ya Dua ambayo iliombwa hapa...

Hivyo hii sio sehemu ya mchezo.. ni mahala pa kutuliza akili na kujitupa kwa Allah kweli kweli. Kukosa rakaa hizi mbili za Nafal ndio kupoteza maana nzima ya Ibada ya Hijja sawa na maagizo ya Mtume s.a.w.. na Allah alivyotuasa..

***Wattakhidhuu Mim maqaami ibraahiima muswallah...*** Na mpafanye mahala aliposimama Ibrahiim kuwa mahala penu pa kusalia...(Quran tukufu 2:126.)

Hakuna atakaye kuwa tayari kupoteza neema za dunia na akhera zinazopatikana mahala hapa.. hiyo hapa ndo mahala pa kujitakasa kimwili na




kiroho.

Mnara huu mdogo mzuri na wa kuvutia ulionakshiwa kwa rangi ya dhahabu, ndipo mahala hasa aliposimama Nabii Ibraahiim a.s kusali wakati wote alipofanya ibada hapa..

Hujaj akipata kusali mahala hapa ni vizur zaidi na akikosa labda sababu ya msongamano, kuna eneo kubwa nyuma mpaka sehemu ya ghorofani na upande wa nje, eneo lote upande huo linaheshimika kama Makaamu Ibraahiim, Hujaji anaweza kusali.

**3. SAFAA NA MAR'WA**

Baada ya Rakaa mbili muhimu pale Makaamu Ibraahiim kukamilika, hapa Hujjaji huelekea katika sehemu nyingine ya Safaa na Mar'wa.

Hapa pamoja na kuendelea kumtukuza Allah Kwa utukufu wake, tunakumbushwa tukio la Bibi Hajira na mwanae Ismail.

Familia hii ya Nabii Ibraahiim a.s na mwanae huyo, waliwekwa mahala hapa wakati Ibraahiim a.s akiwa katika maandalizi ya kuikarabati na kuitakasa nyumba hii ya kuabudia iliyo tukufu kabisa na ya kale zaidi ikiwa ni Ishara na Alama ya Ukuu na Umoja wa Mwenyezi Mungu.

Mahala hapa panapatikana vilima viwili vya Safaa na Mar'wa.

Bibi Hajira akiwa katika bonde hili na mwanae Isamil, alihangaika kwa kutembea na hata kukimbia baina ya vilima hivi akihaha kutafuta maji kwa ajili ya mtoto Ismail aliyekuwa akilia kwa kiu ya maji kutokana na jua kali kabisa na joto lililopo katika eneo hili.




Vilima hivi, asili yake ni mawe ya miamba na kiasi kidogo cha udongo.

Lkn bibi huyo katika kuhangaikia uhai wa mwanae na kuzima kiu ya maji iliyomkabili, akiwa bado ni mgeni katika eneo hili, alikimbia baina vilima hivi viwili kutoka Safaa kwenda Mar'wa, na kutoka Mar'wa kuelekea Safaa-Mara 7 akiamini huenda angepata maji..

Hata hivyo baada ya Maombi na dhikri nyingi za mama huyu, Hatimaye Allah Alipasua chemchem karibu na mahala alipomlaza mwanae huyo.

Wakati huo, eneo hili lilikuwa na mawe na kokoto, jua na joto kali, unaweza kuona hali aliyokumbana nayo Mama huyu.

Lakini kutokana na mazingira na mabadiliko ya ulimwengu pia kukidhi mahitaji ya mamilioni ya watu wanaofika mahala hapa kwa ibada nyakati zote, mazingira yameboreshwa sana.

Hivyo kwa kujifunza yale, Hujaji hukimbia au kutembea Kwa mwendo wa haraka baina ya vilima hivi viwili mara 7 kulingana na mazingira yatakavyoruhusu. Hujaj akianzia Safaa, atakimbia baina ya vilima hivi viwili mara saba, hivyo Kwa mizunguko yote 7 ni sawa na umbali wa kilomita 3 na nusu.

Vile vile katika Masjid Haram kuna wahudumu mbalimbali katika kila idara ambao hutoa maelekezo au hata msaada pale inapohitajika na hususani kwa wenye uhitaji maalumu... (wenye umri mkubwa au walemavu)

***Endelea uk. 11***

## ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA

**NJIA YA UOKOVU NI KUFANYA MAOMBI YA KWELI**

**Hadhrat Masihi Mauud a.s. amesema: "Kumbukeni kuwa kifo ni bora kuliko kuishi maisha yenye dhambi. Ni maisha yenye hatia kubwa. Ni kifo tu ndicho kinachoweza kufupisha kasi ya maendeleo ya dhambi hizo.**

**Lakini hii haimanishi kuwa mtu ajiuwe, bali inatakiwa mtu achukie maisha ya namna hiyo, ajitahidi kuyaepuka kwa kufanya maombi, maombi ya kweli. Hatimaye Mwenyezi Mungu Atamuokoa na dhambi hizo.**

**Ifahamike kuwa maombi (dua) siyo kitu cha mzaha, maombi ni kifo pia, mtu akikubali kifo hiki Mwenyezi Mungu Humuepusha na maisha ya kihalifu yanayosababisha maangamio, badala yake Humpa uhai wenye maisha mema na matakatifu."**

**(Malfuudhat Jal. 3 uk. 616).**

## MANENO YA BUSARA

**Mwanadam anaweza kupata hasara kubwa kama atashindwa kulinda vitu vifuatavyo!**

**{i} IMANI**

**Kama umepoteza imani kwa muumba wako. Na hauaminiki tena ktk jamii yako basi wewe una hasara kubwa sana..Hauwezi kuwa na huruma kama huna imani huwezi kutenda jema kama huna Imani... Imani ni Bora kuliko dini.... Shikilia imani yako chunga isipoteee...**

**{ii} MUDA**

**Tumia muda wako vizuri fanya mambo yenye faida ya leo na kesho.. Tenda yenye kumpendeza Muumba wako..Muda hautasimama ili kukusubiri utimize matakwa yako, Muda hautakusubiri Utubu, Muda hautarudi tena kama utashindwa kuutumia ipasavyo... Heshimu Huu Muda kabla haujageuka kuwa Historia...**

**{iii} ELIMU**

**Kama utapata nafasi ya kupata Elimu na ukashindwa kuitumia vizuri wewe ni mwenye hasara kubwa sana, na matokeo yake utavuna Ujinga...**

**{iv} UPENDO**

**Ikiwa utapoteza Watu au mtu mwenye mapenzi ya kweli kwako kwa makusudi... Ama Hakika utakuwa umepata hasara kubwa sana... Shikilia kwa makini Watu wenye kukupenda na kukujali.....**

**Chunga Usipate Hasara.....**

# Watu Walio Bora Kabisa

*Kutoka uk. 12*

Muminiina. Yeye alikuwa sahaba wa kwanza aliyepewa lakabu ya Amiir ul Muminiina. Historia inaeleza ya kwamba mapenzi ya Allah na Mtume Wake yalimlevya na hakuwa na tamanio lolote ila kujitoa muhanga katika njia ya Mwenyezi Mungu. Ishaq bin Saad bin Abi Waqas anasimulia kutoka kwa baba yake kwamba siku ya vita vya Uhud, Hazrat Abdullah bin Jahsh alimwambia Hazrat Saad njoo tufanye maombi kwa Mwenyezi Mungu. Kwanza Hazrat Saad aliomba hivi E Allah, kesho nikikabiliana na maadui, nipambane na adui aliye hodari kushambulia na mwenye haiba na nipigane naye na nimwue katika njia yako na nichukue silaha zake. Baada ya hapo Hazrat Abdullah bin Jahsh yeye akaomba dua hivi: E Allah ! kesho nipambane na adui mkali na mwenye haiba na nipigane naye kwa ajili yako na anishinde na kuniua na kunikata pua yangu na masikio yangu. Basi nitakapohudhurishwa mbele Yako, uniulize ewe Abdullah ulikatwa pua na masikio kwa ajili ya nani na mimi nijibu kwa ajili yako na Mtume Wako hapo aseme kuwa umesema kweli. Hazrat Saad anasema dua ya Abdullah bin Jahsh ilikuwa bora kuliko dua yangu kwa sababu siku ya mwisho ya vita niliiona maiti yake ikiwa imekatwa pua na masikio. Hazrat Abdullah bin Jahsh na Hazrat Hamza bin Abdul Muttalib walizikwa katika kaburi moja. Khalifa Mtukufu atba alisema: “Sahaba wa pili nitakayemtaja leo ni Hazrat Ka’b bin Zaid ambaye jina lake kamili lilikuwa ni Ka’b bin Zaid bin Qais bin Malik. Yeye alitokana na kabila la Banu Najjaar. Hazrat Ka’b alishiriki katika vita vya Badri na akauawa shahidi katika vita vya Khandaq. Inasemwa kuwa mshale wa Umayya bin Rabia bin Sakhar ndiyo uliomwua. Yeye alikuwa miongoni mwa masahaba walioshiriki mapigano ya Bere Muawwana ambapo wenzake wote waliuawa shahidi isipokuwa yeye. Sahaba wa tatu ambaye nitamtaja leo ni Hazrat Saleh Shukran. Jina lake lilikuwa Saleh lakini lakabu yake ilikuwa ni Shukran. Hazrat Saleh Shukran alikuwa mtumwa wa Hazrat Abdul Rahman bin Aauf mwenye asili ya Kiafrika. Mtume s.a.w. alimnunua ili amhudumie lakini baadhi ya masimulizi yanasema kuwa Hazrat Abdul Rahman bin Aauf alimkabidhi kwa Mtume s.a.w. bila malipo yoyote. Mtume s.a.w. alimwachia huru baada ya vita vya Badri. Hazrat Shukran alikuwa miongoni mwa masahaba wa Suffa. Yeye alipata bahati ya kumkogesha Mtume s.a.w. na kumzika. Hazrat Ibni Abbas anahadithia ya kwamba Mtume s.a.w. aliogeshwa akiwa amevaa shati na Hazrat Ali, Hazrat Fazal bin Abbas , Hazrat Qutham bin Abbas, Hazrat Shukran na Hazrat Aaus bin Khula waliingia katika kaburi lake. Hazrat Shukran anasema ya kwamba wallahi mimi ndiye niliyetandika shuka chini ya maiti ya Mtume s.a.w. kaburini. Hazrat Shukran anaeleza ya kwamba sikupenda mtu yeyote aitumie shuka hiyo baada ya Mtume s.a.w. kupita. Inasimuliwa ya kwamba Hazrat Shukran aliishi Madina lakini alikuwa na nyumba moja huko Basra na akafariki dunia katika zama za Khalifa Mtukufu wa pili, Hazrat Umar ra. Sahaba mwingine nitakayemtaja ni Hazrat Malik bin Dahsham ambaye anatokana na ukoo wa Banu Ghanam bin Aauf wa kabila la Khazraj. Hazrat Malik bin Dahsham alishiriki pamoja na Mtume s.a.w. katika vita vya Badri, Uhud, Khandaqi na vingine vyote. Inasimuliwa ya kwamba Hazrat Utban bin Malik alimjia Mtume s.a.w. na akasema ewe Mjumbe wa Allah, uwezo wangu wa kutazama umepungua na mimi huwaongoza sala watu wangu. Mvua zinaponyesha, mfereji uliopo baina yangu na baina yao hufurika maji na mimi nashindwa kwenda msikitini kwao kuwaongoza sala. Ewe Mjumbe wa Allah! napenda unitembelee na usali sala nyumbani kwangu ili niifanye iwe msikiti. Mtume s.a.w. akasema Inshallah nitakuja. Yeye anaeleza ya kwamba siku moja Mtume s.a.w. na Hazrat Abu Bakar wakaja nyumbani kwangu na wakasali katika kona moja ya nyumba yangu. Watu wa mtaa wangu nao wakaja na kujumuika na mara mmoja wao akauliza “Malik bin Dahsham yuko wapi ? Mmoja wao akaitika kwa kusema yeye ni mnafiki wala hampendi Allah na Mtume Wake s.a.w.. Hapo Mtume s.a.w. akasema msiseme hivyo, je hamuoni ametamka tamko la shahada na anataka kupata radhi ya Allah. Hapo mmoja akasema Allah na Mtume Wake wanajua zaidi lakini sisi huwa tunamwona akiwaelekea na kuwahurumia wanafiki tu. Mtume s.a.w. akasema labda kutokana na upole wa moyo, anataka kuwahubiri wanafiki na kuwaleta karibu na Uislamu. Hazrat Anas bin Malik anasimulia ya kwamba Hazrat Malik bin Dahsham alipolaumiwa mbele ya Mtume s.a.w., Mtume s.a.w. akasema msiwalaumu wenzangu. Khalifa mtukufu alisema “baadhi ya masahaba ambao kuhusiana nao wengine walikuwa na dhana mbaya kuwa pengine wanakanyaga njia isiyofaa hadi wakawaita wanafiki lakini baadaye masahaba hawa hawa ndio walioteketeza makao makuu ya wanafiki kwa idhini ya Allah. Mwenyezi Mungu Aendelee kunyanyua madaraja ya masahaba hawa wa Mtume s.a.w. na pia Atujalie uwezo wa kujichunguza nafsi zetu kuwa sisi tunazifuata amri Zake kwa kiasi gani. Mungu Atusaidie. Amin.

# Safari Ya Umrah

*Kutoka uk. 10*

Mara zote hujaji atakapoifikia mojawapo ya vilima hivi viwili Safaa au Mar’wa huendelea na kumtukuza Allah na akikumbuka Aya hii ya Qur’an na kuisoma:-

Innas safaa wal mar’wata min shaa’irillaah, faman hajjal’bait awi’itamara falaa Junaaha alaih aiyyatawaffaa bihimaa

Yaani “”Hakika Safaa na Mar’wa ni katika Ishara za Mwenyezi, hivyo atakayefanya Hija katika nyumba takatifu au kufanya Umrah, si vibaya kwake kuvizunguka.. (Sura Al baqara)

Kwa ambaye hajakariri Aya hii, karibu na katika kila kilima kuna skrini ya luninga ambayo imefungwa juu ikiwa na Aya hiyo ya Qur’an tukufu inayoelezea vilima hivyo na hivyo hujaji anaweza kusoma pale juu ikiwa anafahamu...

**Zam Zam**

Baada ya kumaliza kukimbia vilima vya Saafa na Marwa, licha ya kujifunza mahangaiko ya Bibi Hajira katika kutafuta maji na kupigania uhai wa mwanae Ismail, hapa pia Hujaji mwili huwa umepata moto na kuchemka, huku jasho jembamba likimtoka.

Ni takriban safari ya kilomita 4



*Mwonekano wa sasa wa njia ya kukimbilia baina ya Safa na Marwa*

akianza na kuzunguka Kaaba na kukimbia baina ya vilima hivi huku mdomoni mwake akimtukuza Mola Mwenye enzi..

Hapa wakati wa faraja umewadia... Hujaji hukaa chini na kupata maji ya Zam zam.

Maji haya ni zawadi toka Kwa Allah baada ya sala na juhudi za Bi Hajira katika kukimbia huku na kule.

Hivyo hujaj hupata baraka hii katika safar ndefu ya Toba na Istighfar.. Safari iliyojaa dhikri, maombi, sala na Tasbih kwa Allah, hatimaye mwili na roho vinaburudika Kwa maji ya Zam zam...

**Kunyoa Au Kupunguza Nywele**

Baada ya kumaliza ibada ya Hajji au Umrah, hujaj hulazimika kunyoa nywele zake au kupunguza kidogo iwapo ana tatizo lolote la kiafya kichwani mwake...

Haya ni moja katika masuala au vipengele muhimu vya Haji..

Baada ya maelezo yale machache, ilikuwa tuanze kuyaangazia maeneo yanayozunguka Masjid



*Kupunguza nywele baada ya ibada ya Umrah*

Haraam ili kujifunza mambo machache, lakini kuna jambo moja kuhusu eneo lile linalozunguka Kaaba. Itakuwa vema kama tukajifunza kitu.

Miaka ya hivi karibuni, Haji imekuwa ikiangukia majira ya joto kali sana, Saudia na nchi jirani za ukanda ule wa ghuba.

Jua kali ambalo huambatana na joto linalofikia nyuzi 40° mpaka 47° ambalo husababisha ardhi kupata moto na hivyo usiku pia kuwa na joto kali..

Kwa ndugu zetu ambao wamehudhuria mwaka jana wanaweza kukumbuka hali ilivyokuwa.

Lakini wakati unaona Hali ni hiyo nje ya Masjidi Haraam, ambapo huwezi kutembea bila viatu hata urefu wa Mita 10 Tu kutokana na ardhi kupata Moto, lakini mambo ni tofauti unapoingia katika eneo linalozunguka Kaaba. Hili ni eneo la wazi pia ambalo jua hulifikia moja kwa moja...

Ajabu zaidi ni Malumalu za eneo Hilo kuwa na ubaridi wakati wote. Sawa na maelezo baada ya kutaka kujua kitu gani kinafanya Malumalu hizo kuwa na ubaridi muda wote na hivyo mahujjaji kuweza kukamilisha kuzunguka Kaaba na hata kusali Makaamu Ibrahim bila joto ambalo huwa limepanda maeneo mengine nje ya Masjidi Haraam..

Moja kati ya niliokuwa nikiwauliza mas’ala mbalimbali kuhusu Masjid Haraam alisema, Malumalu nzito ambazo zimewekwa katika sakafu ile ni maalumu aina ‘THASSOS‘ zilizoagizwa toka Ugiriki ambazo huwekwa kwa mfumo maalumu na hivyo kutoakisi miali ya joto hivyo kuzifanya kubaki katika ubaridi hata jua litawaka kiasi gani...

Kwa kuziangalia ukubwa wake ni kati ya sm 35×90 ambayo inaweza kumtosha mtu mmoja kutumia kama mswala.

Ubaridi wake, humfanya hujjaji kusali Kwa utulivu licha ya joto kali.

Pamoja na ukarabati unaoendelea ndani ya Masjid Haram mpaka sasa, ikiwemo upanuzi wa eneo la Masjid Haraam, uboreshaji wa mifumo ya vipooza joto na ukarabati wa kisima cha zamzam, malumalu hizo zisizoakisi miali ya joto ziliwekwa Januari mwaka jana wa 2017..

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

# MapenziyaMungu

SHAB.-RAMADH.1439AH | JUNI 2018 | IHSAN 1397 HS

**Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w**

Imesimuliwa ya kwamba Hadhrat Abu Hurairah r.a. alisema: Sikumwona yeyote mwenye kushauriana sana na wenzake kuliko Mjumbe wa Allah s.a.w. kushauriana na masahaba zake (Tirmidhi).

# Watu Walio Bora Kabisa

Baada ya *Tashahhud, Taawwudh* na *Surat Faatihah,* Hadhrat Amir-ul Muminiin (atba) alisema: Miongoni mwa masahaba nitakaowataja leo, nitaeleza kwanza habari za maisha ya Hazrat Abdullah bin Jahsh (ra). Mama yake Umaimah binti Abdul Mutalib alikuwa shangazi ya Mtume Muhammad s.a.w.. Kwa hiyo Hazrat Abdullah bin Jahsh alikuwa binamu yake Mtume s.a.w.. Yeye alijiunga na Uislamu kabla ya Mtume s.a.w. kwenda katika Dar e Irqam. Makafiri wa Makka waliitesa sana hata familia yake. Yeye pamwe na ndugu zake wawili Hazrat Abu Ahmad na Abaidullah na dada zake Hazrat Zainab binti Jahsh, Hazrat Umm e Habiba na Hamnah binti Jahsh alifunga safari ya kuhamia huko Habsha (Abyssinia) mara mbili. Hazrat Abdullah bin Jahsh, kabla ya kuhamia Madina alikuja Makka kisha akaenda kwa kabila lake Banu Ghanam na akawachukua watu wote wa Daudaan waliokuwa wameshajiunga na Uislamu na akafika Madina pamoja nao. Yeye aliwahamisha ndugu zake karibu wote huko Makka hadi nyumba nyingi za Makka zikakosa watu na kupigwa kufuli. Hiyo ndiyo hali iliyowakumba Waahmadiyya siku hizi huko Pakistan kuwa baadhi ya vijiji havina watu maana Waahmadiyya wengi wamehama. Ibne Ishaq anasema watoto wa Jahsh bin Riyan walipohama Makka, Abu Sufyan bin Harb alimwuzia Umr bin Alqama nyumba yao. Habari hii ilipomfikia Hazrat Abdullah bin Jahsh, yeye alimjulisha Mtume s.a.w.. Hapo Mtume s.a.w. akasema ewe Abdallah! Je hupendi Mwenyezi Mungu Akujaalie jumba la kifalme peponi badala ya nyumba hiyo? Hazrat Abdullah akajibu, Naam, mimi napenda hapo Mtume s.a.w. akasema basi utapata jumba la kifalme. Safari moja Mtume s.a.w. alimtuma Hazrat Abdullah bin Jahsh pamoja na jeshi fulani kwenye bonde la Nakhla. Habari za tukio hilo zimeelezwa hivi ya kwamba siku moja, baada ya sala ya Ishaa, Mtume s.a.w. alimwambia Abdullah bin Jahsh kuwa kesho nitakutuma sehemu kwa hiyo uje na silaha zako. Siku iliyofuata baada ya sala ya Alfajiri, Mtume s.a.w. akamkuta Hazrat Abdullah bin Jahsh pamwe na silaha zake kama vile mkuki, mshale, upinde na ngao akiwa anamsubiri mlangoni pake. Mtume s.a.w. akamwita Hazrat Ubayye bin Kab na akamwamrisha kuandika barua. Baada ya barua kuandikwa, Mtume s.a.w. akamwita Hazrat Abdullah bin Jahsh na akamkabidhi barua hii na kumwambia nakuteua kuwa kiongozi wa msafara huu. Mtume s.a.w. akimtuma Hazrat Abdullah bin Jahsh alimpa lakabu ya Amiir ul




*Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akitoa hotuba ya Ijumaa kwa waaminio na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.*

*Endelea uk. 11*

# Wakil Mal II Atembelea Tanzania

Na Mwandishi Wetu

Shura ya mwaka huu ilipata msisimko zaidi kwa kuongozwa na mwakilishi wa Khalifatul Masih wa V ambaye alikuwa katika ziara ya kutembelea Afrika.

Wakil Mal II, Bwana Mir Rafiq Mubarak alipata fursa ya kutembelea mikoa mbalimbali ya nchi yetu ikiwemo Pwani katika matawi ya



*Wakil Mal II akizungumza na wanajamaat wa Dar es salaam*

Bungu, Kibiti, na Ikwiriri napo Morogoro ambapo alipata fursa ya kukitembelea Chuo chetu cha Ualimu Jamia Ahmadiyya pamoja na shule za



*Wakil Mal II akizungumza na wanajamaat wa Iringa*

msingi na awali za Ahmadiyya, pia alifika katika hospitali yetu na Studio za MTA zilizopo Morogoro Mjini. Pia alizuru katika baadhi ya matawi



*Wakil Mal II akiwahutubia wajumbe wa Shura Kitonga*

ya mkoa wa Iringa. Hapa jijini Dar es salaam aliyatembelea makaburi ya Wasia na shule ya sekondari ya Ahmadiyya iliyopo Kitonga, nje kidogo ya jiji ambapo Shura ya Taifa pia ilifanyika.

Wito wake katika ziara hiyo ilikuwa ni kuwahimiza wanajamaat na



*Wakil Mal II akizuru makaburi ya Wasia Temeke, Dar es salaam*

mpango wa Wasiyyat. Kwa msaada wa Allah mwitikio ulikuwa wa kutia moyo.

Wakil Mal II pia alipata fursa ya kuongoza kikao cha Shura kilichoisha kwa mafanikio makubwa.

Subhana'llah! 'Waislamu' Wavunja Msikiti Pakistani Uk. 3